SportPesa
TZS. 878,152,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#

UKURASA 3

**WAWILI** wapitishwa kumrithi Maalim ACT- Wazalendo




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Januari 29, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580840
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Mambo 4 utata kifo cha askari mahabusu

**BABA** wa marehemu aibua mazito, amtaka IGP...

*Endelea ukurasa 2*



## TANESCO yatangaza rasmi mgawo wa umeme

UKURASA 3



## Shahidi wa Jamhuri kesi ya Mbowe apata wakati mgumu

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAIKABILI MBAO UK.24
MAONI, KATUNI UK.6




Ofisa Mpango wa kudhibiti magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele katika Wizara ya Afya, kitengo cha usubi, Oscar Kaitaba (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kilele cha maadhimisho ya magonjwa hayo kitakachofanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square kesho. Kushoto ni Isaack Njau kutoka Kitengo cha Kichocho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mambo manne utata kifo askari mahabusu

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na kifo cha aliyekuwa Ofisa wa Jeshi la Polisi mkoani Mtwara, Grayson Mahembe, anayedaiwa kujinyonga akiwa mahabusu, baba yake mzazi ameeleza mambo manne yenye utata juu ya tukio hilo.

Mahembe alikuwa miongoni mwa maofisa wa polisi waliokuwa wanashikiliwa kwa tuhuma za mauaji ya mfanyabiashara wa madini, Mussa Hamisi (25) mkazi wa Kijiji cha Ruponda, Nachingwea mkoani Lindi, aliyeuawa Januari 5, mwaka huu.

Inadaiwa kuwa askari hao walimpora mfanyabiashara huyo madini yenye thamani ya Sh. milioni 70 kisha kumuua kwa kumchoma kwa sindano ya sumu na hatimaye kumtupa katika kitongoji cha Majengo, kijiji cha Hiari wilayani Mtwara.

Kutokana na kifo cha ofisa huyo, baba yake mzazi, Gaitan Mahembe, amefunguka na kusema hajaridhishwa na taarifa za kifo cha mtoto wake, huku akimwomba Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, kuingilia kati.

Akizungumza juzi Tabata Segerea jijini Dar es Salaam alipohojiwa na kituo kimoja cha televisheni, baba mzazi wa kijana huyo ambaye ni ofisa mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), alisema: "Nilipewa taarifa kwamba mwanao ameshikiliwa kwenye mahabusu ya polisi tarehe 22 (Januari). Baadaye nikapigiwa simu kwamba bahati mbaya amefariki (dunia) amejinyonga akiwa mahabusu. Ilinishtua kidogo."

"Hatua ambazo walizochukua wao walifanya jambo haraka haraka. Kidogo wakaniuliza mwili upelekwe wapi? Ameandika kwao ni Iringa, nikawaambia ninakaa Dar es Salaam, uletwe Segerea."

Kutokana na kauli ya mzazi, mambo kadhaa yameibua utata kuhusu kifo cha askari huyo yakiwamo;-

**NDUGU KUTOSHIRIKISHWA**

Mzee Mahembe ameibua hoja kwamba kuna usiri mkubwa juu ya kifo cha mwanawe ambaye ameacha mjane na mtoto mdogo kutokana na ndugu wa karibu kutokushirikishwa baada ya tukio la kujinyonga.

Alisema jambo lililoishtua familia ni kwamba walipewa taarifa baada ya kijana wao kuwa tayari ameshafariki dunia kwa kile kilichoelezwa na jeshi la Polisi kwamba amejinyonga.

Kutokana na hali hiyo, Mzee Mahembe alihoji iwaje wapigiwe simu na kuelezwa kuwa tayari mwili uko katika chumba cha maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mtwara ya Igula wakati hata ndugu mmoja hakushirikishwa ili kuthibitisha kwamba alijinyonga.

**MWILI KUTOPIGWA PICHA**

Suala lingine alilohoji kutokana na utata wa kifo hicho ni mwili kutokupigwa picha kuthibitisha kuwa mtoto wake amejinyonga.

Mzee Mahembe alisema kutokuwapo kwa picha iliyopigwa na polisi na familia kuonyeshwa kuwa alipoteza maisha kwa njia zilizoelezwa na polisi kunazidi kuleta utata na maswali yasiyo na majibu.

Alisema polisi walipaswa kupiga picha na upande wa ndugu wa marehemu kuitwa kushuhudia kabla ya kuondolewa.

"Polisi walete picha waonyeshe marehemu alikuwa amejinyonga. Ndiyo maana ninamwomba IGP alifafanue. Inasemekana ukweli wake ndiyo uliomponza na ukweli wake ndio uliosababisha hata hao wengine wasemwe," alisema huku akifafanua kwamba Grayson alisema kwa nini ateseke peke yake wakati alikuwa anatekeleza maagizo ya wakubwa wake?

**MKANGANYIKO MAJERAHA**

Jambo lingine linalozusha utata juu ya kifo hicho, kwa mujibu wa baba wa marehemu ni mkanganyiko kuhusu majeraha shingoni waliyoonyeshwa ndugu mwili ukiwa katika chumba cha maiti.

Polisi katika taarifa yao, walisema Grayson alifariki dunia kwa kujinyonga kwa kutumia dekio lililokuwa ndani ya mahabusu hiyo huku ndugu wakitakiwa kushuhudia majeraha ya kamba shingoni wakati mwili uko mochwari.

"Lakini kwa ufupi ndugu waliitwa ikiwa tayari marehemu ametolewa kutoka kwenye tukio kupelekwa hospitalini. Ndugu yetu amekwenda kuona mwili ukiwa hospitalini na kuonyeshwa hapa (shingoni) kuna michubuko ya kamba.

"Hapo kukawa na mkorogano ya kwamba ni kamba si tambala la dekio kama walivyosema. Sasa kwenye mahabusu kuna tambala la dekio, siyo mahabusu ya uraiani ni mahabusu ya wao wenyewe polisi.

Kidogo imenisumbua akili, sijaridhishwa na familia yote haijaridhishwa, ninaomba majadiliano, IGP afafanue ukweli, afuatilie na ukweli uwe wazi," alisema Mzee Mahembe

**MWILI KUSHUSHWA HARAKA**

Akisimulia zaidi, alisema watu hao walifika nyumbani kwake, Tabata Segerea, wakiwa na mkuu wa msafara na wakaingiza gari na kutaka mwili ushushwe haraka haraka. Hatua hiyo pia inaibua utata kwa nini jambo hilo lifanyike kwa namna hiyo?

"Niliwaambia hatuupokei. Ilikuwa vurugu nusura tuanze kupigana, nikawaambia tunaomba mwili huu ukahifadhiwe halafu waje tuzungumze hapa. Wakaenda kuhifadhi Hospitali ya Jeshi la Polisi iliyoko eneo la Kilwa Road.

"Tuliwaambia safari yetu ni Iringa lakini hatutaupokea mpaka tupate ukweli wa tukio lenyewe, mbaya zaidi ninajua sheria," alisema.

**KUSAFIRISHWA, KUZIKWA KIRAIA**

Mzee Mahembe pia alisema kilichowashangaza zaidi ni mwili wa kijana wao ambaye ni ofisa wa polisi kusafirishwa kiraia wakati alipaswa kusindikizwa kijeshi kama sheria na taratibu zinavyotaka.

"Hata IGP aseme yule ni ofisa wa jeshi, ilitakiwa asindikizwe kijeshi na akazikwe kijeshi. Hilo halikufanyika amekwenda kama mtu wa kawaida. Ninachoomba uchunguzi ufanyike," alisisitiza.

Kutokana na mkanganyiko huo, Mzee Mahembe alisema kama kuna uwezekano, wanaomba kumpata mwanasheria awasaidie kupata ukweli kwa sababu hakuna picha hata moja inayoonyesha Grayson alikuwa amening'inia amejinyonga.

# Shahidi wa Jamhuri kesi ya Mbowe apata wakati mgumu

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 12 katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu amekuwa na wakati mgumu baada ya kubanwa na mawakili wa utetezi wakiongozwa na Peter Kibatala.

Luteni Dennis Urio, shahidi aliyekuwa akitegemewa kwa hamu kutokana na kubeba maudhui ya kesi hiyo, alipata wakati mgumu baada ya kuambiwa hakutokea Morogoro kwenda mahakamani bali katokea katika kambi fulani ya jeshi alikokuwa ametekwa.

Urio pia katika mahojiano hayo alidai kwamba hakuna ujumbe katika mawasiliano yake na Mbowe juu ya kushambulia viongozi wasiopenda upinzani wala kulipua masoko na vituo vya mafuta.

Alidai hayo jana katika Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga wakati akihojiwa na Kibatala na Dickson Matata.

Wakili Kibatala alimwambia shahidi kwamba wakati anakuja mahakamani hakutokea Morogoro, alitokea kwenye kambi fulani ya Jeshi alikokuwa ametekwa na kushindwa kujibu.

Wakili Kibatala pia alimwelekeza shahidi kusoma Yohana Sura ya 8 mstari wa 31 hadi 39 na Waefeso Sura ya 4 mstari wa 25 hadi 32.

Shahidi huyo alisoma na baada ya hapo aliulizwa mistari hiyo ina maana gani ndipo akadai: "Biblia inasema tusiogope tuseme kweli na mwingine unasema tusiseme uongo na tupendane."

Luteni Urio alidai kuwa anajua maisha ya washtakiwa Halfani Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya kuwa yako mikononi mwake.

Alidai kuwa taarifa za Mbowe kutaka amtafutie vijana atakaokuwa nao kuchukua dola alimshirikisha DCI (Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai) na kwamba katika Jeshi la Wananchi Tanzania hakuna kitengo kinachoshughulika na ugaidi.

Pia alikiri kwamba Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mgulani ilikuwa karibu kwenda kutoa taarifa za Mbowe kuliko kwa DCI alikokwenda.

Shahidi akiendelea kuhojiwa na Wakili Kibatala alidai wakati anaonyeshwa simu zake nne zilizotolewa mahakamani kama kielelezo, hakutambua simu moja moja kwa IMEI namba zake.

Alidai katika ushahidi wake hakumwambia Jaji kwa nini alishindwa kumweka Mbowe chini ya ulinzi.

Luteni Urio pia alidai kuwa hakumbuki siku aliyokwenda ofisini kwa DCI na kwamba alikwenda kuonana na Mbowe Mikocheni kwa kuwa alimfahamu kwa kumwona kwenye televisheni.

Shahidi alidai alimwarifu bosi wake kuhusu mahitaji ya vijana ya Mbowe Agosti 5, 2020 lakini alikiri hafahamu sheria yoyote inayomruhusu kutafuta vijana wa kutekeleza mipango ya kigaidi.

Hata hivyo, alidai kuwa hakumuonyesha Jaji sAkihojiwa na Wakili Dickson Matata, Luteni Urio alidai hautapatikana ushahidi wa maandishi, sauti au ujumbe mfupi wa maandishi unaoweza kuthibitisha kwamba Mbowe alimwambia anataka vijana wa kumsaidia kuchukua dola.

Shahidi huyo alidai kuwa hakuna mahali ujumbe unasema kushambulia viongozi ambao hawapendi upinzani wala hakuna mahali unasema kulipua masoko na vituo vya mafuta.

Pia alidai kuwa Mbowe hakumtajia vituo vipi vya mafuta vinataka kulipuliwa na kiongozi yupi anayekusudiwa kudhuriwa.

## HABARI KITAIFA

# Tahadhari mvua kubwa mikoa saba

**Na Faustine Feliciane**

MKOA wa Dar es Salaam ni miongoni mwa mikoa saba iliyotahadharishwa kuchukua hatua kutokana na uwezekano wa kupata mvua kubwa kuanzia leo mpaka Jumatatu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) iliyotolewa jana, mvua hizo pia zitaathiri mikoa ya Morogoro, Pwani (ikihusisha pia Mafia), Ruvuma, Lindi, Mtwara na Zanzibar.

"Kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Ruvuma na Zanzibar, mvua hizi tunatarajia zitanyesha siku ya Jumapili (kesho)," alisema mtaalamu wa Hali ya Hewa kutoka Mamlaka hiyo, Joyce Makweta.

Alisema Hali hiyo itaendelea mpaka Jumatatu ambapo athari za wastani zinatarajiwa kutokea kutokana na mvua hizo.

"Watu wachukue tahadhari kwa sababu tunatarajia baadhi ya shughuli za kiuchumi zinaweza kusimama na hata baadhi ya makazi kuzungukwa na maji lakini pia kunaweza kutokea uharibifu wa miundo mbinu, tunaomba wananchi kuendelea kufuatulia taarifa za utabiri unaotolewa na Mamlaka na kuchukua hatua," alisema Makweta.

Alisema TMA inaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na itakuwa ikitoa taarifa kila itakapohitajika.

Mvua zinazoendelea sasa kwa baadhi ya mikoa, alisema ziko nje ya msimu na zinatokana na mgandamizo mdogo wa hewa mashariki mwa visiwa vya Madagascar na kupelekea unyevunyevu kuja katika maeneo ya Tanzania.

Hata hivyo, alisema maeneo mengine yanaendelea kupata mvua zilizo ndani ya msimu ambazo utabiri wake ulitolewa mwishoni mwa mwaka jana.



Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim, Stanley Kafu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa droo kubwa ya kuwatafuta washindi wa kampeni ya 'Weka Mkwanja Tukutoe!' ambapo Taasisi ya Work of Mary (Focolare Movement Tanzania) ya mkoani Iringa iliibuka mshindi wa zawadi kuu gari aina ya Toyota Vanguard. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Wateja Wadogo na Kati wa benki hiyo, Andrew Lyimo na Meneja Msaidizi wa Bidhaa za Rejareja, Callist Butinga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yatangaza mgawo wa umeme

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limetangaza kuanza mgawo wa umeme kwa siku 10 katika baadhi ya maeneo kutokana na kupisha marekebisho ya uboreshaji wa miundombinu ya nishati hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mgawo huo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, alisema mgawo huo utaanza Februari Mosi hadi 10, mwaka huu. Alisema ratiba maalumu ya mgawo huo itatolewa leo.

Chande alitoa taarifa hiyo wakati akikagua utekelezaji wa upanuzi wa Kituo cha Kinyerezi I.

Alisema wakati uboreshaji ukifanyika itawalazimu kuzima mitambo mingine kupisha kazi hiyo na kwamba katika kipindi hicho, kuna maeneo yatakuwa na upungufu wa umeme kutokana na mitambo kutokupata gesi ya kutosha.

"Katika hizo siku 10 kutakuwa na upungufu si nchi nzima, ni baadhi ya maeneo kwa sababu tunayo mitambo mingine na tutatoa ratiba kuonyesha ni maeneo gani yataathirika kuanzia kesho hadi tarehe 10 ili wananchi wajipange katika shughuli zao za kiuchumi," alisema Chande.

Pia alitaja chanzo cha kukatika kwa umeme katika baadhi ya maeneo kuwa ni kutokana na upungufu wa umeme unaosababishwa na ubovu wa miundombinu, uchakavu wa mitambo na ukame.

Alisema katika jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa umeme unaboreshwa, TANESCO inaendelea na maboresho ya vituo vya kuzalisha umeme vikiwamo Kinyerezi I, kinachozalisha megawati 185 na Ubungo III megawati 112.

"Mpaka sasa uzalishaji katika mitambo ya Ubungo III umefikia megawati 60 ambazo tayari zimeunganishwa kwenye gridi ya taifa. Katika upanuzi wa Kinyerezi I megawati 70 za awali zitaingia kwenye mfumo wa gridi Aprili, mwaka huu.

"Pia ifikapo Agosti, mwaka huu, kazi hiyo itakuwa imekamilika na kukiwezesha kituo cha Kinyerezi I ambacho kwa sasa kinazalisha megawati 150 kuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 335," alisema Chande.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa mitambo inayoongezwa ili kuzalisha umeme, itasababisha mahitaji ya gesi asilia kuongezeka na kwamba imewalazimu kufanya uboreshaji wa mfumo wa gesi kwenye mifumo ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Pan African Energy Tanzania (PAET). Alibainisha kuwa uboreshaji huo utafanyika kwenye visima vya gesi vilivyoko Songosongo kuanzia Februari Mosi hadi 10, mwaka huu, huku akisema kukamilika kwa kazi hiyo kutahakikisha gesi ya ziada inayohitajika inapatikana. Pia alisema utekelezaji wa maboresho hayo utasababisha upungufu wa gesi katika mitambo ya kuzalisha umeme wa gesi asilia na kuzimwa kwa baadhi ya mitambo hiyo ili kupisha maboresho.

Meneja wa Mradi wa Upanuzi wa Kinyerezi I, Mhandisi Abdallah Kiyoko, alisema katika utekelezaji huo hadi kufikia Aprili, megawati 70 zitakuwa tayari na zilizobakia 115 zitakamilika Julai na kukiwezesha kituo chote kuwa na megawati 185.

Alisema upanuzi huo ni wa kituo cha megawati 150 ambacho kikikamilika kitakuwa na megawati 335 huku akibainisha kuwa kwa sasa wanaendelea na ufungaji wa mitambo na ujenzi wa barabara ambayo itawezesha vifaa vizito kupitishwa na kufungwa katika kituo hicho.

# Wawili wapitishwa kumrithi Maalim Seif

**Na Christina Mwakangale**

HALMASHAURI Kuu ya ACT-Wazalendo, imepitisha majina ya wanachama mawili kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa wa chama, kujaza nafasi ya Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia Februari, mwaka jana.

Wanachama waliopendekezwa ni Juma Duni Haji na Hamad Masoud Hamad, ambao watapigiwa kura leo katika Mkutano Mkuu wa chama hicho utakaofanyika Dar es Salaam.

Katibu Mwenezi na Uhusiano kwa Umma wa chama hicho, Salim Bimani, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema kikao hicho kilichokuwa na asilimia 80 ya wajumbe waliohudhuria, kilipokea mapendekezo ya Kamati Kuu iliyokutana juzi.

Alisema mapendekezo hayo yaliwasilishwa Halmashauri Kuu ili kujadiliwa ikiwamo kuitisha mkutano mkuu leo ambao una ajenda kadhaa ikiwamo kuwasilishwa majina ya wanaowania nafasi ya mwenyekiti wa chama taifa.

Sambamba na hayo, alisema mkutano mkuu pia utawapigia kura wanachama wanaowania nafasi ya makamu mwenyekiti ambao ni Othman Masoud Othman na Juma Said Sanani.

"Halmshauri Kuu imepokea majina na kuwapitisha Juma Duni Haji na Hamad Masoud Hamad. Kesho (leo) wataingia kwenye mkutano mkuu katika kinyang'anyiro na wagombee, na kumpata mmoja wapo kujaza nafasi ya marehemu Maalim Seif Sharif Hamad," alisema Bimani.

"Pia majina yanayowania nafasi ya makamu mwenyekiti, Halmashauri Kuu, imewapitisha Othman Masoud Othman na Juma Said Sanani."

Aliongeza kuwa mchakato wa kuanza kuwaniwa kwa nafasi tofauti kwenye chama hicho ulianza Januari 4 hadi 17, mwaka huu, ili kutoa nafasi kwa wagombea kuchukua fomu kwa nafasi tatu, uenyekiti, makamu mwenyekiti na ujumbe wa Halmashauri Kuu.

Wanachama 11 walitia nia kugombea, huku nafasi ya ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa- Tanzania Bara, ikiwaniwa na wanachama saba wakiwamo Chrisant Msipi na Ester Thomas.

Wengine ni Fungo Benson, Johnson Gagu, Msafiri Mtemelwa, Jafet Masawe na Fidel Christopher.

Chama hicho, Februari 17, mwaka jana, kiliondokewa na aliyekuwa Mwenyekiti wake wa Taifa, Maalim Seif Sharif Hamad.

# Halmashauri tisa kikaangoni makusanyo kiduchu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ameziweka kikaangoni halmashauri tisa ikiwamo jiji la Mbeya kutokana na kukusanya mapato ya ndani chini ya asilimia 50.

Mbali na Mbeya, halmashauri zingine zilizowekwa kikaangoni ni Ubungo na Morogoro na ameziitaka kuwasilisha maelezo ndani ya siku 14 kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuhusu sababu za kushindwa kufikia malengo ya makusanyo.

Bashungwa alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu mapato na matumizi ya ndani ya halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021.

"Wakuu wa mikoa wahakikishe kuwa halmashauri zote ambazo zimekusanya chini ya asilimia 50 ya lengo la mwaka la makusanyo ya ndani, zinawasilisha maelezo kwa katibu mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuhusu sababu za kushindwa kufikia lengo baada ya kusomwa kwa taarifa hii," alisema Bashungwa.

Waziri alisema maelezo hayo pia yabainishe mikakati ya jinsi ya kuboresha mapato ya ndani katika kipindi cha nusu mwaka kilichosalia (Januari - Juni, 2022).

Akitoa taarifa hiyo ya mapato alisema katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2021/22 Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, imeongoza kwa kukusanya asilimia 102 ya makisio yake ya mwaka, ikifuatiwa na Kaliua, Shinyanga na Mlele ambazo zimekusanya kwa asilimia 91.

"Halmashauri za wilaya ya Bumbuli na Kilindi zimekuwa za mwisho katika kundi hili kwa kukusanya asilimia 27 ya makisio ya mwaka, zikifuatiwa na halmashauri ya wilaya ya Bunda ambayo imekusanya kwa asilimia 28," alisema.

Kwa kundi la halmashauri za miji, alisema katika kipindi hicho, Halmashauri ya Mji wa Korogwe imekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 39, ikifuatiwa na Halmashauri ya Mji wa Nzega asilimia 42 na Mji Masasi pia kwa asilimia 42. "Katika kundi la halmashauri za Manispaa kwa kipindi cha nusu mwaka, Kahama imeongoza kwa kukusanya mapato kwa asilimia 67 ikifuatiwa na Musoma asilimia 65 na Ilemela asilimia 55.

"Katika kundi hili Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, imekuwa ya mwisho kwa kukusanya imekusanya asilimia 37 ya makisio yake ya mwaka ikifuatiwa na Kigoma/Ujiji asilimia 38 na Ubungo asilimia 40," alisema.

Kwa kundi la majiji, alisema Jiji la Tanga limeongoza kwa kukusanya mapato kwa asilimia 56 huku Arusha ikishika nafasi ya pili kwa asilimia 55 na Mwanza asilimia 54.

Katika kundi hilo, alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya imekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 45 ya makisio ikifuatiwa na Jiji la Dar es Salaam asilimia 52 huku Dodoma ikiwa na asilimia 53.

Kutokana na hali hiyo aliwaagiza wakuu wa mikoa wasimamie na kuhakikisha hoja zote za ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinajibiwa, zihakikiwe na wakaguzi ili kufungwa na kupunguza mzigo wa hoja kwa halmashauri.

"Pia hatua stahiki zichukuliwe kwa wote waliosababisha hoja za ubadhirifu wa fedha za umma," alisema.

Bashungwa pia aliwataka wakuu wa mikoa wazisimamie halmashauri, ili kuandaa makisio ya mapato ya ndani yenye uhalisia kulingana na fursa zilizopo kwenye halmashauri zao ikiwa ni pamoja na kuibua vyanzo vipya vya mapato na hatimaye kuongeza mapato na kuboresha utoaji wa huduma.




Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Christopher Newton kutoka Dawati la Jinsia na Watoto la Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, akielimisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za Kata ya Mwananyamala, kuhusu jinsi ya kuzuia udhalilishaji na unyanyasaji wa kingono, wakati wa utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na vitendo hivyo, unaoratibiwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Msajili atoa suluhisho utitiri migogoro ardhi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

KATIKA kuhakikisha mlundikano wa mashauri ya migogoro ya ardhi unapungua nchini, Msajili wa Mabaraza ya Ardhi, Stela Tullo, amewataka Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba wa Wilaya kusikiliza mashauri katika wilaya zingine ambazo hazina wenyeviti.

Akizungumza katika Maonesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea jijini Dodoma, Tullo alisema lengo ni kutatua migogoro ya ardhi kwa wakati na haraka sambamba na kusogeza huduma karibu na wananchi.

"Katika kusogeza huduma karibu na wananchi, tumeamua kusogezea huduma karibu wananchi. Tumejiwekea mikakati na kuelekeza wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba wa wilaya kwenda wilaya zingine ambazo hazina wenyeviti kusikiliza mashauri ya wananchi na si wananchi kuwafuata wenyeviti waliko," alisema.

Kwa mujibu wa Msajili, kwa sasa kuna mabaraza 72 yanayotoa huduma na kati ya hayo 28 hayana wenyeviti waliopangiwa vituo katika wilaya hizo na kufanya wenyeviti wa wilaya za jirani kwenda kufanya kazi huko.

"Katika mabaraza 28 ambayo hayana wenyeviti, kuna ratiba tumewapangia kwenda kusikiliza mashauri kwenye wilaya hizo. Jambo hilo linawapunguzia wananchi mzigo wa kusafiri kutoka wilaya moja kwenda nyingine," alisema.

Maonyesho ya Wiki ya Sheria yalianza Januari 23, mwaka huu na kufunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi na yanatarajiwa kufikia kilele leo.

# Mbaroni tuhuma mauaji mhudumu gesti

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma limemkamata Azizi Makangira (39), mkazi wa Kiyanga Manispaa ya Mtwara Mikindani kwa tuhuma za kumuua aliyekuwa mhudumu wa nyumba ya kulala wageni mjini Songea.

Mtuhumiwa anadaiwa kumkaba shingo kisha kumfunga kamba za viatu shingoni Gema Haule (23), aliyekuwa mhudumu wa Peace Lodge iliyoko kata ya Matarawe, Manispaa ya Songea.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Pili Mande, alisema jana ofisini kwake kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa Januari 18, mwaka huu, majira ya saa 10:00 jioni kwenye nyumba hiyo kisha kutokomea kusikojulikana kwa kutumia usafiri wa bodaboda.

Kamanda Mande alisema mtuhumiwa huyo alifanya hivyo baada ya kushindwa kulipa kodi ya pango Sh. 50,000 kutokana na kukaa kwa siku tano katika nyumba hiyo ya wageni.

Alisema Haule alikutwa ndani ya chumba namba 4 kwenye nyumba hiyo akiwa ameuawa kwa kunyongwa kwa kamba ya viatu baada ya mtuhumiwa huyo kufika kudai mali zake zilizokuwa zimezuiwa na mmiliki wa nyumba.

Kwa mujibu wa Mande, baada ya kutenda kosa hilo, mtuhumiwa alikimbia lakini polisi walipopata taarifa, walifika kwenye eneo la tukio na kuanza uchunguzi mara moja na Januari 22, mwaka huu, walimkamata mtuhumiwa na sasa yuko mahabusu kwa upelelezi zaidi.

Wakati huo huo, Polisi mkoani Ruvuma, katika kijiji cha Mchuruka wilayani Tunduru, wamemkamata mwanamke (jina limehifadhiwa) mwenye umri miaka 34, akiwa na vipande 34 vya nyamapori aina ya swala nyumbani kwake.

HABARI KITAIFA

# Kesi kupinga Ndugai kujiuzulu yatupwa

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetupilia mbali kesi ya kupinga kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika wa Bunge Job Ndugai, baada ya kubaini alifuata utaratibu katika kuchukua uamuzi huo.

Shauri hilo la kikatiba lililofunguliwa na Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi, James Mbatia, lilitupwa jana mbele ya jopo la majaji watatu likiongozwa na Jaji John Mugeta. Majaji wengine katika shauri hilo walikuwa Benhaji Masoud na Sekedia Kisanya.

Mbatia alifungua kesi ya kikatiba namba 2 ya mwaka 2022 chini ya hati ya dharura akipinga kujiuzulu kwa Ndugai akidai hakufuata utaratibu kwa mujibu wa Ibara ya 149(1) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jaji Mugeta, katika uamuzi huo, alisema mahakama imepitia hoja zilizowasilishwa na pande zote mbili na kuona kwamba madai ya Mbatia hayana msingi wowote, hivyo yanatupwa kwa kuwa Ndugai alifuata utaratibu katika kujiuzulu kwake.

"Hakuna shaka kwamba ibara ya 149 ya Katiba ya Tanzania inatoa taratibu ambazo Spika anatakiwa azifuate wakati anataka kujiuzulu. Bunge ni taasisi yenye maofisa wenye wajibu wa kutekeleza shughuli za kila siku na miongoni mwa maofisa hao ni Katibu wa Bunge.

Kwa mujibu wa ibara ya 149 (2) ametajwa Katibu wa Bunge kwamba taarifa ya kujiuzulu Spika inaweza kuwasilishwa kwakwe. Kama Ndugai alikuwa na nia ya kujiuzulu, Bunge siku hiyo halikukaa kikao awasilishe wapi taarifa siku hiyo?" alihoji Jaji Mugeta.

Alisema kwa mujibu wa ibara hiyo, mtu aliyetajwa ni Katibu ndiye aliyepokea barua ya kujiuzulu kwake siku hiyo, hivyo aliwasilisha kwa mtu sahihi.

Mahakama hiyo ilisema Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, wakati anawasilisha hoja zake, pia alidai Ndugai aliwasilisha nakala ya barua ya kujiuzulu kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Januari 6, 2022 siku ambayo alijiuzulu.

"Ilikuwa halali Ndugai kuwasilisha nakala ya barua yake ya kujiuzulu kwa Katibu Mkuu wa chama chake kwa sababu chama chake ndiyo mdhamini wake wakati alipogombea nafasi ya Uspika "Mahakama imebaini kwamba wakati mdai (Mbatia) anafungua shauri lake mahakamani, hakuwa na taarifa kwamba Ndugai alipeleka taarifa hiyo kwa Katibu wa Bunge na inawezekana angekuwa na taarifa hiyo asingekuja mahakamani," alisema Jaji Mugeta. Alisema Ndugai aliandika barua ya mkono kwa Katibu wa Bunge na barua ya pili aliwasilisha kwa Katibu Mkuu wa CCM. Jaji alimpa Mbatia nakala ya barua hiyo mahakamani ili ajiridhishe.

Jopo hilo lilisema kwamba hakuna Mtanzania aliyeiona barua ya Spika kujiuzulu na iliyokuwa ikisambaa ni taarifa kwa umma iliyotolewa na CCM.

Alisema mahakama imebaini shauri lililofunguliwa halina msingi linatupwa na kila upande ubebe gharama zake.

Mleta maombi katika shauri hilo la kikatiba ni Mbatia, mjibu maombi namba moja alikuwa ni Ndugai, namba mbili Katibu wa Bunge na watatu Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).



Waziri wa Sheria na Katiba, George Simbachawene, akizungumza katika mkutano na Menejimenti ya watendaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, alipofanya ziara katika ofisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri: Utaratibu mbovu chanzo ucheleweshaji kesi

Na Romana Mallya

WAZIRI wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, amesema ucheleweshaji wa kesi za serikali ulitokana na mawakili wa serikali kutokuwa na uratibu mzuri na kushindwa kujipanga.

Simbachawene aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali kuona shughuli zinazofanyika.

Akizungumza na watumishi katika ofisi hiyo, aliwakumbusha kuwa kazi yao ni kukuza diplomasia, uhusiano na kuhakikisha haki inatendeka na hakuna mtu wala serikali anaonewa.

Pia aliwaeleza kuwa kulinda haki ya uchumi hakuchagui kwamba ni serikali au ni nani amefanya kosa.

"Kazi ya ofisi yako (Wakili Mkuu wa Serikali) ni kuhakikisha sekta binafsi inalindwa na inatoa mchango wake katika ujenzi wa uchumi. Kila kitu kwa zama za leo ni uchumi. Hii kazi mnayoifanya ni sehemu muhimu ya kujenga uchumi na uchumi ndio unaojibu maswali yetu. Uchumi ndio unaoleta maendeleo," alisema.

Pia aliipongeza ofisi hiyo kwa kitendo chake cha kuokoa Sh. Bilioni 236.6 kwa miezi tisa tu.

"Sikutegemea kuona mafanikio makubwa takriban miezi tisa mmeweza kuokoa Sh. bilioni 236.6 kwa kuisaidia serikali kushinda mashauri lakini pia usuluhishi wa mashauri mbalimbali," alipongeza.

Simbachawene alisema hilo ni jambo la kujivunia kwa sababu kwa kuokoa fedha hizo wanajihakikishia pale wanapozungumza jambo lolote waweze kusaidiwa.

Alisema hata viongozi wakuu akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan anajua umuhimu wa ofisi hiyo ndiyo maana kila wanachoomba wanapewa.

"Katika kipindi cha miezi tisa Rais Samia ameshawapa magari takribani 16 pia mmepata watumishi tutaendelea kusema zaidi, na maombi yenu mnayoomba yataendelea kufikiriwa," alisema.

Pia alisema ilipokuwa kitengo ndani ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bajeti yake ilikuwa zaidi ya Sh. bilioni 80 lakini walipojitegemea imeshuka na kuwa Sh. bilioni 12.

"Upungufu ule ni mkubwa mno, ninadhani majukumu ni makubwa kuliko kipindi kilichopita, serikali hii ya awamu ya sita ambayo inafungua milango ya uwekezaji.

"Inafungua milango ya kujenga uchumi wa kisasa hasa tukizingatia tumeingia uchumi wa kati ulioleta muingiliano mkubwa wa uwekezaji wa ndani na nje lazima mashauri na usuluhishi utakuwa mwingi na kazi hii itafanywa na nyie," alisema.

# Serikali yajizatiti kukabili selimundu

Na Christina Mwakangale

SERIKALI imesema itajikita katika kubadili mwelekeo wa kukabiliana na ugonjwa wa selimundu nchini, ikiwamo kutoa elimu kwa jamii na kutoa huduma ya vipimo kwa watoto wachanga mara baada ya kuzaliwa.

Imesema vipimo vya mapema mara baada ya mtoto kuzaliwa, vitabainisha iwapo mtoto ana selimundu na kuanza matibabu mapema ambayo kwa kiwango kikubwa yatapunguza vifo vitokanavyo na ugonjwa huo.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof Abel Makubi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, kwenye Kongamano la Kisayansi la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), lililolenga kujadili mwelekeo mpya wa mapambano na udhibiti wa selimundu nchini.

Alisema, wakati huu ugonjwa huo bado ni janga kutokana na Tanzania kuwa kati ya nchi tano barani Afrika zilizo na mzigo mkubwa wa watoto wanaozaliwa na selimundu, ambao ni takribani 11,000 kila mwaka.

"Tanzania ni miongoni mwa mataifa matano yaliyo na idadi kubwa ya wagonjwa na bado kuna unyanyapaa kuhusu ugonjwa huu. Nchi zingine ni Angola, Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na India. Utafiti unaonyesha asilimia 17 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya selimundu na wengi hawajijui hali zao," alisema Prof. Makubi.

"Selimundu inachangia asilimia saba ya vifo vyote vya watoto walio na umri wa miaka mitano, ikimaanisha katika watoto 100 wanaofariki dunia saba ni kutokana na selimundu. Kiwango hiki ni kikubwa, serikali itashirikiana na taasisi, wadau kupunguza athari hizi," aliongeza.

Mratibu wa Mradi wa Selimundu MUHAS, Dk. Agnes Jonathan, alisema tayari watoto 5,000 wamepimwa na kuwaingiza kwenye mfumo wa tiba na kuwafuatilia kwa karibu.

"Tunawapima watoto wachanga mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza kubaini mapema kama wana tatizo ili waanze kupata tiba mapema, ugonjwa huu ambao unatokana na kurithi vinasaba," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Andrea Pembe alisema MUHAS ilianza kufanya utafiti wa ugonjwa huo kuanzia mwaka 2004, lengo likiwa kuwabaini mapema na kuanza matibabu wanaougua selimundu.

Alisema iwapo wakibainika mapema wanaougua ugonjwa huo itakuwa rahisi kufuata ushauri wa kitabibu pamoja na kuishi maisha marefu pamoja na kuwa na tatizo hilo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba inahitaji maandalizi mazuri michuano ya CAF

**MISEMO** ya kale inasema kwamba, haijalishi ni wakati gani mgumu unaopitia, lakini mara zote kuna nyakati nzuri zitakuja tu mbele yako.

Au kwa maana rahisi ni kwamba, kwenye kila jambo gumu, kuna jambo zuri zaidi linakuja hapo mbeleni.

Hivyo ndivyo tunavyoweza kusema kwa sasa kwa upande wa Klabu ya Simba ambayo ni wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, lakini inapitia kipindi kigumu kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania bara.

Simba katika mechi tatu zilizopita za Ligi hiyo, imeambulia pointi moja, huku ikipoteza kwenye mechi mbili na hivyo kujikuta wakipitwa pointi 10 na vinara Yanga ambao ni watani zao wa jadi.

Ilianza kufungwa na Mbeya City kule kwenye uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga, halafu ikatoka sare na Mtibwa Sugar pale Manungu Morogoro na baadae ikachezea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa walima miwa Kagera Sugar.

Matokeo hayo ambayo ni mabaya kwa Simba kwenye Ligi Kuu sio kiashiria kizuri kuelekea kwenye mechi za michuano ya CAF Februari na hivyo ni lazima ichukue hatua za haraka kujipanga na kujiandaa vizuri.

Nipashe tukiwa kama mmoja wa wadau wakubwa wa soka hapa nchini, tunaona kwamba, pamoja na matatizo yote ambayo Simba inaonekana kupitia, lakini viongozi, wachezaji, wanachama na wapenzi wanatakiwa kutambua kwamba wana wajibu mwingine wa kijitathmini na kujipanga kwenye mechi za kimataifa.

Simba imepangwa kundi moja la D pamoja na timu za RS Berkane kutoka Morocco, ASEC Mimosas ya Ivory Coast na US Gendarmerie ya Niger na timu zote hizo zinafahamika sio za kuzichukulia kimzaha.

Simba mechi yake ya kwanza kwenye kundi hilo itaanzia nyumbani dhidi ya ASEC Mimosas Februari 13 mwaka huu kwenye dimba la Benjamin Mkapa. Halafu Februari 20 itakuwa ugenini nyumbani kwa Gendarmerie nchini Niger kabla ya kucheza tena ugenini Februari 27 dhidi ya Berkane kule Morocco.

Machi 13 itakuwa katika dimba la Benjamin Mkapa kurudiana na Berkane, halafu Machi 20 kuwa ugenini kucheza na ASEC Mimosas na itamaliza mechi za hatua hiyo ya makundi kwa kurudiana na Gendarmerie hapa nyumbani.

Ukiangalia ratiba ya mechi hizo za makundi, Simba ina ahueni moja ya kuanza nyumbani, lakini bila maandalizi ya kutosha hilo linaweza lisisaidie, kwani timu itakayoanza nayo ni moja kati ya kongwe kwenye mashindano hayo. Hivyo basi Nipashe tunaona kwamba, benchi la ufundi pamoja na wachezaji wenyewe wanatakiwa kujiandaa kisaikolojia na kujituma kwenye mazoezi kwa ajili ya mechi hizo.

Mchezo wa soka ili ushinde ni lazima ufanye maandalizi ya kutosha kwa mazoezi na kuwafanya wachezaji wako kuwa fiti kimwili na kiakili, bila vitu hivyo uwezekano wa kupata ushindi unakuwa ni mgumu sana.

Hivyo sisi tunatoa wito kwa Simba kuichukulia michuano hiyo kwa umuhimu mkubwa na maandalizi yake yawe ya hali ya juu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kupenya kwenye kundi lao.

Ikumbukwe kwamba, Simba imeangukia kwenye michuano hii ya Shirikisho baada ya kutolewa kule kwenye Ligi ya mabingwa Afrika, hivyo tunaamini wataitumia nafasi hii vizuri kwa kufanya vyema kwenye mashindano hayo.


Simba inapaswa kujua kwamba ina jukumu kubwa la kuiwakilisha vizuri Tanzania katika mashindano hayo ambayo ni ya pili kwa ukubwa kwa ngazi ya Klabu barani Afrika ukiacha yale ya Ligi ya mabingwa.

Tunaamini kwamba, Simba ambayo ina wachezaji wenye vipaji inaweza kukabiliana vizuri na changamoto inazozipitia kwa sasa na kujipanga vizuri tayari kwa ajili ya michezo hiyo hatua ya makundi.

Nipashe tunaamini kuwa kujipanga na kujiandaa vizuri kwa Simba kunaweza kuwafanya wapate matokeo mazuri kwenye hatua hiyo na kusonga mbele kutoka hatua ya makundi.

Tuna imani viongozi wa Simba watalitazama hilo kwa umakini mkubwa kwenye maandalizi ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano hiyo ya CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji wengi Simba viwango vimeshuka

Na Adam Fungamwango

**MWAKA** 1976 Simba ilitwaa Ubingwa wa Tanzania Bara ambao mwaka mmoja nyuma ulikuwa unashikiliwa na Yanga. Simba iliushikilia ubingwa huo kuanzia mwaka huo kwa miaka mitano hadi 1981 ilipofungwa na Yanga bao 1-0, lililowekwa wavuni ya Juma Mkambi 'General'.

Huo ukawa mwisho wa enzi wa Simba, baada ya miaka mitano ya mfululizo wa ubingwa. Ilikuwa na wachezaji mahiri kama kina Athumani Mambosasa, Daudi Salum, Mohamed Kajole. Nico Njohole, Thuwein Ally, Adam Sabu, Jumanne Hassan 'Masimenti', George Kulagwa, Abdallah Mwinyimkuu, Martin Kikwa, Mohamed Bakari 'Tall' na wengine wengi ambao huko nyuma si tu walitetemesha soka la Tanzania, bali Afrika nzima.

Baadhi ya wachezaji hao walikuwepo mwaka 1974 Simba ilipofika nusu fainali ya Klabu Bingwa Afrika na hata wale waliokwenda kupindua mechi nchini Zambia kwa timu ya Mufulira Wanderers mwaka 1979, ilipokwenda kushinda ugenini mabao 5-0 na kusonga mbele, wakati wiki mbili nyuma ilitoka kufungwa mabao 4-0 nchini Tanzania. Ni moja kati historia zisizofutika kwenye soka la Afrika.

Pamoja na umahiri wao wote, baada ya kipigo na kuukosa ubingwa, viongozi wa klabu ya Simba wakafanya maamuzi magumu. Wakawapa mkono wa kwaheri wachezaji wengi wa timu hiyo, wenye majina makubwa, na kuanza kuingiza damu changa lakini wenye uwezo wa kusakata kabumbu, timu ikaanza kukaa sawa.

Hata msimu huu hali ni hiyo hiyo. Ukiwaangalia wachezaji wengi wa Simba ni wale wale walioipa Simba mafanikio makubwa miaka minne nyuma, Ubingwa wa Tanzania Bara, Kombe la FA na kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mara mbili. Wakapata majina makubwa.

Lakini ukweli lazima usemwe kuwa kwa sasa wengi wao viwango vyao vimeshuka. Si wale tena tunaowajua. Wamebaki na majina yao makubwa kutokana na kazi kubwa waliyoifanya huko nyuma.

Ikifika wakati mchezaji wa timu kubwa Afrika kama Simba, kutuliza mpira inakuwa tatizo, huwezi kushangaa timu ikifungwa.

Wanachama na mashabiki wa Simba wamekuwa wakitafuta mchawi kwa nini timu yao inafanya vibaya, wengine wakidai timu inakamiwa sana, wengine wakidai 'kamati za ufundi' hazifanyi kazi vizuri na vingine vinavyofanana na hivyo.

Lakini kwa jicho langu la kiufundi, pamoja na mambo mengi wanayoyasema, inawezekana yapo, timu kama ya Simba, wachezaji wake wakiwa fiti kama ile ya miaka miwili mitatu iliyopita, hata mtu afanye vipi, watakufunga tu.

Leo timu zote za Ligi Kuu haziogopi tena kucheza na Simba, wakati miaka miwili mitatu iliyopita si timu za Tanzania tu, hata Al Ahly, Mabingwa wa Afrika, walikuwa wanaogopa kucheza nayo.

Niwe mkweli tu, kuwa wachezaji kama John Bocco, Shomari Kapombe, Mzamiru Yassin, Hassan Dilunga, Chris Mugalu, wameshuka viwango sana na hawawezi tena kuisaidia timu hiyo, huku Bernard Morrison na Rally Bwalya wakicheza soka la kishule na kitoto zaidi badala ya kutafuta matokeo.

Sitaki kwenda mbali sana, na wala siwezi kuwapa lawama viongozi wa Simba kwa nini hawakufanya usajili kipindi cha dirisha dogo. Kile ni kipindi ambacho huwezi kupata wachezaji wazuri wa kusajili ambao hawana timu. Utabambikiwa tu. Labda kwa sasa cha kufanya ni kocha kuanza kuwaamini kina Jimson Mwanuke, Yusuph Mhilu, Denis Kibu, Isael Mwenda, kuungana na wachezaji wengine wanaoonyesha uwezo na kuibeba timu kwa sasa kama Pape Sakho, Henock Inonga, Joash Onyango, Mohamed Hussein, Jonas Mkude na Clatous Chama.

Ipate ubingwa au isipate, hiyo ni kengele ya hatari kuwa sasa klabu inatakiwa kuondoa wachezaji wengi baada ya msimu kumalizika kwa sababu viwango vyao vimepungua sana kutokana na umri, kubweteka, kutojituma au kulewa mafanikio kwani kila kitu tayari wameshakipata, ubingwa na kufanya vema kimataifa.

Simba inatakiwa kufanya usajili mkubwa baada ya ligi kumalizika na kuondoa wachezaji wengi wa ndani ambao hawana msaada kabisa, pia kutafakari nafasi 12 za wachezaji wa kigeni, ilete wenye uwezo mkubwa na hadhi kama ya klabu hiyo.

# Shaka atoa siku 30 ZAWA kupeleka maji

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** ZANZIBAR

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ametoa mwezi mmoja kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama katika mradi wa tangi la Kikwajuni.

Alitoa agizo hilo akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 Kikwajuni Mkoa wa Mjini Unguja, ikiwa ni sehemu ziara ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa visiwani Zanzibar.

Alisema kutofanyia kazi kwa ufanisi miradi iliyotumia fedha za wananchi kutekelezwa ni kumhujumu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Shaka alisema ni vizuri miradi ikatekelezwa kwa wakati badala ya kuichonganisha serikali na wananchi jambo ambalo chama hawawezi kulikubali.

Aidha, alisema CCM inazo taarifa za ziada kuhusu kutofanya kazi kwa mradi huo uliotarajiwa kuleta ahueni kubwa ya huduma ya maji safi kwa wananchi.

Alisema taarifa hizo zinaonyesha kuna mikono ya baadhi ya watu wasiotaka mradi ufanye kazi kwa maslahi yao.

Shaka alisema serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya nane, inafanya kazi kubwa kuleta maendeleo, hivyo CCM haitakubali kuona jitihada hizo zikiwekewa vizingiti na baadhi ya watu.

Awali Mbunge wa Kikwajuni ambaye pia ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuph Masauni, alikiomba CCM kisaidie kusukuma mradi huo ili utoe maji baada ya juhudi zao kugonga mwamba kwa muda mrefu.

Masauni alisema mradi huo umetekelezwa kwa fedha nyingi ambazo yeye binafsi na viongozi wenzake walihangaika kuzitafuta kwa wafadhili na tangi kujengwa na miundombinu kukamilika ingawa bado haujaanza kutoa maji.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Dk. Salha Mohamed Kassim, alikiri mradi kutofanya kazi kwa muda mrefu ingawa umekamilika na kwamba hilo linatokana na chanzo kilichotarajiwa kujaza maji katika tangi hilo kutokuwa na uwezo kwa sasa kutosheleza ujazaji maji.

Alisema ipo mikakati ya dharura ya kuhakikisha tangi hilo linajazwa maji kwa ajili ya kupeleka huduma kwa wananchi wakati jitihada za kupata maji ya kutosha kulijaza kama ilivyokusudiwa zikiendelea kufanyika.

# Mfumo kupima utendaji kazi kufumuliwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imesema imebaini upungufu kwenye mfumo wa utendaji kazi na tathimini katika ngazi ya mtumishi (OPRAS) na inakusudia kuufanyia marekebisho ili kuongeza tija.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema hayo jana alipozungumza na wakuu wa idara wa ofisi hiyo jijini hapa.

Mhagama alisema serikali imebaini upungufu uliomo kwenye mfumo huo, hivyo inakusudia kuufanyia marekebisho ili kuleta tija kwa watumishi wa umma.

Alizitaja baadhi ya kasoro katika mfumo huo kuwa ni pamoja na kusanifiwa kwa fomu ambazo zilitumika kwa kada zote na taasisi zote bila kujali mazingira ya utendaji kazi wa eneo husika.

Waziri alisema matumizi ya mfumo huo yanalazimisha watumishi kutumia muda mwingi kujaza makaratasi katika hatua zote za utekelezaji wa mfumo hivyo kutokuwa rafiki kwa watumiaji.

Aliongeza upungufu mwingine ni baadhi ya watumishi kutokujaza fomu hizo kwa wakati au kujaza fomu za miaka tofauti mfululizo kulingana na matukio ya kiutumishi.

Mhagama alisema katika kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, hatua kadhaa zimechukuliwa na zingine zinaendelea ili kuhakikisha wanakuja na mfumo bora zaidi na wenye tija na kuondoa upungufu uliokuwamo.

Pia alisema mfumo huo mpya wa kielektroniki unatarajiwa kuanza kutumika kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, hivyo kuwataka watendaji wakuu wote wa taasisi za umma kufanya maandalizi ya kusimamia mfumo huo kikamilifu.

Kadhalika alisema mfumo huo mpya utakuwa na manufaa mengi kwa watumishi wa umma kwa kurahisisha uandaaji wa mikataba ya utendaji kazi na kwamba unawataka viongozi na wasimamizi kutimiza wajibu wao katika kufuatilia, kupima na kutoa mrejesho wa utendaji wa watumishi .

Alitaja mifumo mingine ambayo inaendelea kuboreshwa kuwa ni mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara, mfumo wa mpango mkakati ,mfumo wa mkataba wa huduma kwa mteja,kumbukumbu na masijala.

Mifumo mingine ni utendaji kazi na tathmini katika ngazi ya taasisi tathmini ya hali ya rasilimali watu, vibali vya kusafiria nje ya nchi ,mawasiliano serikalini na mfumo wa upokeaji wa mrejesho wa utoaji huduma pamoja na mfumo wa sema na waziri wa Utumishi.

Alisema lengo la mifumo yote hiyo ni kuwawezesha watumishi na wananchi kuwasiliana moja kwa moja na waziri ili kutoa malalamiko au maoni yao kuhusu masuala ya utumishi na utawala bora.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi (wa pili kulia), akionyeshwa mchoro wa eneo litakalojengwa viwanda katika Kijiji cha Panga Tupu, wakati wa ziara ya Wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja juzi. **PICHA: FAHAD ASRAJI**

# Ummy mgeni rasmi magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele.

Magonjwa hayo ni pamoja na usubi, kichocho, minyoo ya tumbo, trakoma/vikope, matende na mabusha.

Mratibu wa Kitaifa wa Mpango wa Taifa wa Kuratibu Magonjwa hayo katika Wizara ya Afya, Dk. George Kabona, alisema jana kuwa kilele cha maadhimisho hayo yaliyoanza Januari 24 ni kesho Januari 30 ambayo imetengwa kimataifa kuadhimisha magonjwa hayo.

Alisema maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila mwaka yatafanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square mkoani hapa na kuhudhuriwa na wageni mbalimbali.

Tanzania, alisema ni miongoni mwa mataifa yaliyoathiriwa na magonjwa hayo na imekuwa ikitekeleza mpango wa kuyatokomeza hivyo kila mwaka hutenga wiki ya kuadhimisha.

Alisema lengo la siku hiyo ni kujikumbusha kwamba nchi inawajibu wa kutokomeza magonjwa hayo na kusherehekea mafanikio ambayo yamepatikana katika kuyadhibiti.

"Tunaangalia mafanikio kiasi gani tumepata na kujaribu kuondoa changamoto zilizopo kwa pamoja ili tuweze kufikia malengo kutokomeza magonjwa haya ifikapo mwaka 2030 ili yaondoke kabisa kwenye jamii yetu," alisema.

Dk. Kabona alisema kuna magonjwa mengi nchini ambayo yalikuwa hayapewi kipaumbele lakini kuna matano ambayo yameathiri kwa sehemu kubwa ambayo kwa miaka 10 serikali imekuwa ikipambana nayo.

Alisema magonjwa hayo yako sehemu kubwa hapa nchini na yameathiri Watanzania wengi ikiwemo kichocho ambacho kimeonekana kuathiri zaidi watu wengi.

Mratibu huyo alisema udhibiti wa magonjwa hayo ulianza miaka mingi iliyopita lakini mpango wa taifa wa kuyadhibiti kwa pamoja ulianza mwaka 2009. Alisema magonjwa hayo yaliunganishwa pamoja ili yadhibitiwe pamoja kwa sababu yote yanafanana kwa kuathiri na madhara yake yanaonekana baada ya miaka mingi.

"Madhara yake si kiafya tu. Yanasababisha unyanyapaa kwa jamii na katika mifumo ya kutolea afya hayapewi kipaumbele kiasi kwamba mtu akipata magonjwa haya akienda hospitali si rahisi kupewa huduma," alisema

Dk. Kabona alisema kupitia mpango huo ulioko Wizara ya Afya, serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa kuhakikisha inahamasisha watu wayatambue na mifumo ya afya iimarishwe.

Alisema serikali imekuwa ikitoa elimu kupitia njia mbalimbali ili watu waweze kujikinga na magonjwa hayo ili wasipate madhara ambayo huwa yanatokea taratibu.

# Bashungwa ataka halmashauri kuingizwa kwenye mpango

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ameagiza halmashauri zote nchini ziingizwe katika mpango kabambe wa kuboresha miji.

Alitoa maagizo hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akipokea taarifa ya Mradi wa Kuendeleza Miji Mkakati (TSCP) katika majiji na manispaa nane, Mradi wa Ukuzaji na Uboreshaji wa Miji (ULGSP) katika miji 18, Mradi wa Uboreshaji na Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) katika wilaya tatu.

Taarifa hiyo ilitolewa na timu ya wataalamu, inayosimamia miradi inayotekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) na kusimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

"Katika taarifa yenu nimesikia kuwa mipango kabambe imeandaliwa kwenye halmashauri zilizonufaika na mradi tu kwenye miji 18, majiji na manispaa pamoja na halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam.

"Lakini kwa namna miji yetu inavyokua kwa kasi mpango kabambe unatakiwa kuandaliwa kwenye halmashauri zote nchini, hivyo mjenge hoja kwenye miradi inayokuja ili halmashauri zilizobakia nazo ziweze kuwa na Master Plan," alisema Bashungwa.

Alisema lazima serikali iwe mbele ya mipango ya wananchi, miji ipangwe mapema ili wananchi wakute mpango wa matumizi bora ya ardhi na kusitokee athari yeyote baadaye ya kiuchumi au kisaikolojia kwa wananchi.

Aidha, aliwashauri wataalamu hao kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi kwa lugha ya kiswahili ili kupata maoni kutoka kwa wahusika wakuu wa miradi ambao ni wenyeviti wa vijiji, watendaji na madiwani.

Bashungwa akikagua Daraja la Jangwani, alihimiza usafi wa mazingira na kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuhakikika mitaa na barabara zinakuwa safi.

Alisema TAMISEMI itazungumza na wasimamizi wa sera ambao ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuangalia namna ya kutoa elimu ya usafi kwa wanafunzi shuleni ili kuepuka uchafu wa mazingira ikiwamo mito.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gongwe, alipongeza kazi kubwa inayofanywa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, alishauri serikali ijenge vituo vya daladala katika masoko ya kisasa yaliyojengwa ili kupeleka wateja na kuongeza mzunguko wa biashara.



Mkurugenzi Mtendaji wa DKT International Tanzania, Kelvin Hudson (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Cycle for HIV 2022', yenye lengo la kuhamasisha vijana uelewa wa kujilinda na Ukimwi, ambapo kutakuwa na shindano la kutambua bidhaa za kampuni hiyo na washindi kwenda Zanzibar kushiriki mbio za baiskeli. Kushoto ni Mkuu wa Idara ya Masoko DKT, Farida Rubanza na Balozi wa Bull Condom, Calisah Abduhamid. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kunenge awapa matumaini wawekezaji

**N Julieth Mkireri,** PWANI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amefanya ziara kwenye baadhi ya viwanda mkoani humo na kukutana na wawekezaji ambao amewaahidi kushughulikia kero zao na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Akizungumza baada ya kutembelea baadhi ya viwanda hivyo vilivyoko katika Wilaya ya Kibaha na Mkuranga, alisema ziara yake inalenga kukagua hali ya uzalishaji kwenye viwanda hivyo na vikwazo wanavyokumbana navyo.

Akiwa katika viwanda vya Lake ambavyo vinatengeneza matangi ya mafuta, mabomba, matangi ya maji na mitungi ya gesi, alielezwa kikwazo cha umeme mdogo ambao haukidhi mahitaji wakati wa uzalishaji. Kunenge aliwaeleza wawekezaji katika viwanda alivyotembelea kuwa serikali inahimiza uwekezaji kwenye sekta ya viwanda hivyo imejipanga kutatua vikwazo vinavyokwamisha malengo ya wawekezaji.

"Ziara yangu hii ni kukagua uzalishaji na kusikiliza kero za wawekezaji tuzitafutie ufumbuzi wa haraka, Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ipo kwa ajili ya kutatua vikwazo na kuendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda tutahakikisha mazingira yanaboreshwa," alisema.

Ofisa mwajiri wa Lake Group, Fadhil Msemwa, alishukuru Kunenge kwa ziara yake ya kusikiliza kero za wawekezaji na kuomba ziara hizo ziwe endelevu kwani zinawapa motisha kuona namna serikali inavyowajali.

Pia alikwenda Mkuranga katika kiwanda cha nondo cha Fujian Hexingwang.

## Hospitali ya CCBRT yasaidiwa vifaa

**Na Mwandishi Wetu**

HOSPITALI ya CCBRT imepokea msaada wa vifaa mbalimbali vilivyotolewa na Taasisi ya RYTHM Foundation Tanzania, ili kusaidia kwenye shughuli mbalimbali.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo, Mkuu wa Kitengo cha Uuguzi,Emelda Lwena, alishukuru na kusema msaada huo wa mashuka, taulo za kike, shani, sukari, vijiko, neti pamoja na vitu vingine vinavyogharimu shilingi milioni 7 ni muhimu katika jitihada za hospitali hiyo kubadili maisha ya watu.

Alieleza kuwa tangu mwaka 2003, CCBRT imefanya upasuaji kwa wanawake 10,000 wenye fistula bila malipo.

"Tangu 2003, CCBRT iliondoa gharama zote za matibabu kwa wagonjwa wa fistula, kwa kufanya hivyo tumeweza kuondoa kikwazo kikubwa kwa wagonjwa wengi ambao wasingeweza kupata matibabu."

Lwena alisema "Kwa niaba ya CCBRT, ningependa kuwashukuru QNET kwa msaada wenu na ukarimu, hii imedhihirisha kujitoa kwenu katika kazi hii ya kubadili maisha ya watu. Tunatiwa moyo na watu mbalimbali wenye moyo wa ukarimu na wakujitolea kama wenu."

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Meneja wa QNET Ukanda wa Sub-Sahara Afrika Biram Fall, alisema msaada huo umelenga kufikia jamii ya watu ambao wamesahaulika na wenye uhitaji sambamba na falsafa ya kampuni ya RYTHM
(Jiinue Ili Kumsaidia Mwanadamu).

Aliongeza kuwa msaada huo pia unaakisi matakwa ya kampuni ya ushirikiano katika masuala ya kijamii na kuleta matokea chanya.

"Umaskini unawaweka watu katika hatari ya kupata maambukizi mbalimbali na kuwaathiri sana," ameeleza.

Alisema kutokana na janga la Covid-19, watu wengi wamepoteza vyanzo vyao vya kujipatia kipato na wanaishi kwa mashaka makubwa.

"Tumefanya kidogo tunachoweza kurudisha tabasamu na furaha kwa wale wanaohitaji zaidi," alieleza Fall.

**"Tangu 2003, CCBRT iliondoa gharama zote za matibabu kwa wagonjwa wa fistula, kwa kufanya hivyo tumeweza kuondoa kikwazo kikubwa kwa wagonjwa wengi ambao wasingeweza kupata matibabu."**



## Majaji watakiwa kuhamia Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimi Juma, amewataka majaji kuanza kujitayarisha kuhamia Dodoma kwa kuwa suala hilo halikwepeki na ni lazima litekelezwe.

Prof. Juma alibainisha hayo wakati akiweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama jijini Dodoma.

Alisema majaji wote wanapaswa kujiandaa kwa sababu mwakani jambo hilo litafanyika na halina kukwepa kwa sababu wengi wao wameshahamia mkoani Dodoma.

"Nawaomba mkae mkao wa kula kwa sababu suala la kuhamia Dodoma halina mjadala. Ni lazima litekelezeke," alisema Jaji Mkuu.

Alisema jengo hilo linatarajiwa kukamilika Desemba 2022 ili siku ya sheria mwakani na shughuli za kimahakama zianze kufanyika.

Pia alisema ile hofu ya Jaji Mkuu Mstaafu Othman Chande ya kusema amesikitika kustaafu huku mahakama ikiwa haina makao makuu, iondoke kabisa kwa sababu ndoto yake tayari serikali imeitimiza.

Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, alisema anashukuru ushirikiano unaoonyeshwa baina ya Mahakama na Wizara yake ambao anaamini utaleta mafanikio makubwa katika kazi.

Alisema kwa muda mfupi alioingia katia wizara hiyo amepewa ushirikiano wa kutosha na mahakama kiasi kwamba anajiona yupo katika wizara ileile aliyokuwa mwanzo.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema anawashukuru makandarasi wa ujenzi wa jengo hilo huku akiwaomba waendelee kuwa na moyo huyo.

Alisema jengo hilo mpaka kukamilika litagharimu kiasi cha Sh. bilioni 129.5 ambapo hadi sasa wameshamlipa mkandarasi Sh. bilioni 47.2.

# Jafo asema uharibifu wa mazingira umechangia kuwapo mgawo wa maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema uharibifu wa mazingira umechangia kwa kiasi kikubwa mgawo wa maji katika miji mbalimbali.

Jafo aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kati ya wadau wa mazingira na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kujadili masuala ya utunzaji mazingira na upandaji miti.

Alisema uharibifu wa mazingira umekuwa sababu kuu ya kupungua kwa kiwango cha maji katika vyanzo vya maji katika maeneo mengi ya nchi.

"Hivi karibuni tumeshuhudia mgawo wa maji katika jiji la Dar es Salaam kutokana na kiwango cha maji kupungua katika chanzo cha Ruvu Chini na Ruvu Juu. Hali hiyo ilisababisha maji yaliyopo kushindwa kukidhi mahitaji ya watu katika maeneo hayo," alisema.

Pia alisema Bwawa La Mindu mkoani Morogoro lilikauka na kusababisha Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kukumbwa na uhaba mkubwa wa maji.

Jafo alisema ili kuikabili hali hiyo, wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri wanatakiwa kusimamia kampeni ya kitaifa ya upandaji miti ambayo itasaidia kutunza mazingira.

"Mabadiliko ya tabianchi si suala la kusimuliwa. Tumeshuhudia ukame uliosababisha mifugo mingi kufa kutokana na ukosefu wa maji na malisho hapa Dodoma. Mvua katika msimu huu zimechelewa kuanza, zimeanza kunyesha kama siku tatu zilizopita," alisema Jafo.

Alisema serikali pamoja na wadau wa mazingira wanao wajibu wa kubainisha nini kifanyike ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Leo (juzi) tumeitana hapa ili kuona ni kwa namna gani Dodoma inakuwa ya kijani na kuondoa 'poor coordination' (uratibu mbovu) ya kila mtu kufanya kazi hii kivyake. Lakini pia kubadilishana mawazo na wadau na ni imani yetu kuwa mkutano huu utatoa tija kubwa sana," alisema.

Pia aliwahimiza wananchi kutumia msimu huu wa mvua kupanda miti huku akibainisha kuwa malengo ya serikali ni kupanda miti milioni 276 kwa mwaka.

"Wakuu wa mikoa na wilaya wasimamie upandaji miti pamoja na kuwatumia wanafunzi kila mmoja kuwa na mti wake ambao atautunza na kwa idadi ya wanafunzi wa nchi nzima tunatarajia kupanda miti takribani milioni 14.1," alisisitiza Jafo

Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Andrew Komba, alisema lengo la kikao hicho ni kukutana na wadau ili kujadiliana namna ya kuifanya Dodoma kuwa kijani ikiwa ni kuunga mkoani kampeni ya kukijanisha Dodoma iliyozinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati huo akiwa Makamu wa Rais.



Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi wa Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari (TEHAMA) wa Mahakama ya Tanzania, Kalege Enock, alipotembelea banda la Mahakama, kwenye maonyesho ya Wiki ya Sheria Kitaifa katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mameneja Posta mikoa watakiwa kuwa mabalozi anwani za makazi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, ameagiza mameneja wa mikoa wa Shirika la Posta Tanzania kuwa wajumbe wa kudumu kwenye vikao vinavyosimamia utekelezaji mradi wa kuweka mfumo wa anwani za makazi na postikodi ili ukamilike kwa muda uliopangwa.

Nape aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa 28 wa Baraza la Wafanyakazi wa Shirika hilo kwa mwaka 2022/23.

Alimwelekeza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kupeleka maelekezo maalumu kwenye mikoa kwa kuwa viongozi hao ni watu muhimu kushirikishwa ili kufanikisha mradi kukamilika Mei, mwaka huu, badala ya miaka mitano kama ilivyokuwa imepangwa awali.

"Hili jambo ni lenu wengine wafanye kuwasaidieni lakini ninyi ndio mwongoze jambo hili. Sasa inawezekana mliwekwa pembeni au mlikaa pembeni sasa mwenye sekta anasema twendeni jikoni. Katibu Mkuu simamia warudi jikoni kihalali kwa nyaraka na kwa taratibu wapewe heshima inayostahili," alisema.

Nape alisema uamuzi wa huduma za posta kiganjani utasaidia kuifanya Tanzania kuwa ya kidigitali.

Kadhalika, alisema sera ya shirika hilo imekuwa ya muda mrefu na kwa sasa kuna maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kupitia sera zote ili ziendane na wakati wa sasa wa kidigitali.

Aliagiza usimamiaji wa haki za wafanyakazi kwenye shirika hilo kwa kuwa si vyema wakanung'unika.

"Niwaahidi Wizara ninayoisimamia nataka iwe wizara ambayo waliopo hawataki kutoka na wengine wanatamani kuja kufanya kazi kwa kusimamia haki za watu. Bahati nzuri mimi na Katibu Mkuu tumepitia milima na mabonde ya kutosha tunajua umuhimu wa haki za watu. Huku sisi tutasimamia na nyie mkasimamie," alisema.

Alipongeza mapendekezo ya mpango mkakati wa nane wa kibiashara 2022-2026 wenye lengo la kufanya posta ya kidigitali kwa biashara endelevu yanayoendana na maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan na matakwa ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu.

"Tutaendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa shirika. Nimesoma taarifa yenu kuna baadhi ya maeneo kuna madeni madeni malimbikizo ya kodi, migogoro ya mambo ya maslahi niwaahidi mzigo mkubwa mlioubeba sasa mnyamwezi kaja tutaupeleka pale unapostahili, kwa sehemu kubwa serikali ina wajibu kubeba madeni haya na nguvu ya kuyabeba ninayo.

"Nia na sababu ya kubeba ninayo, niwahakikishie tumejipanga kubeba huu mzigo mambo yaende sawa. Tutazungumza na wenzangu na Hazina ili msiendelee kubeba mzigo huu. Kwenye siasa kule wakati mwingine watu wakishindana sana wanatumia magoli ya mkono kama refa hajaona goli ni goli. Kwa hiyo kwa gharama yoyote na hili tutalifunga msijali,"alisema.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi, alisema umoja wa watumishi wa posta umesaidia kutatua kero mbalimbali na kwasasa Shirika linakua kiuchumi na taswira imezidi kuwa bora.

Kaimu Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo, alisema mkutano huo utajadili utekelezaji wa majukumu ya taasisi na maslahi ya watumishi.



# Vikwazo vya wanawake kukosa fursa bayana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk Malik Akil, amesema wanawake wanakosa uwezeshaji katika masuala ya kiuchumi na ushiriki katika demokrasia.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mdahalo wa nafasi za wanawake katika ngazi za uamuzi na ushiriki wao katika masuala ya kidemokrasia. Mdahalo huo umeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar na umefanyika Maisara, Zanzibar.

Dk. Malik alisema kuna mambo ya msingi yanaweza kuinua maendeleo ya wanawake ambayo yanapaswa kuzingatiwa, ikiwamo wanawake kuchangamkia fursa zinazopatikana katika maendeleo. Alisema badala ya wamawake hao kufanya hivyo, wanategemea fursa hizo kuambiwa na wanaume.

Aliwataka kutowategemea wanaume kwa sababu baadhi ya wanaume hawapendi maendeleo ya wanawake.

Katibu Mkuu alisema bado wanawake wana uoga katika kugombea nafasi za uongozi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kupewa vitisho na wanaume wanapojaribu kugombea nafasi hizo hasa nafasi za kisiasa.

"Niwaombe wanawake msiwe woga katika kuomba nafasi za uongozi. Msitishwe na wanaume, panapoongozwa na mwanamke hapaharibiki kitu. Wanaume sisi tuna madudu mengi yakiwamo ubadhirifu na rushwa," alisema.

Dk. Malik alisema kuongozwa na wanawake ni baraka kwa sababu wamekuwa na hofu katika ubadhirifu wa mali na ni aghalabu sana kuwakuta wakijihusisha na rushwa.

Pia alisema nafasi za uteuzi wa Rais zinahitaji sifa na uwezo, hivyo ni vyema kusoma na kujifunza ili kuwa na uwezo wa kuwa kiongozi na kutoachwa nyuma zinapotokea nafasi za uteuzi.

Alisema serikali imeanza kutoa fursa nyingi kwa wajasiriamali kwa kupatiwa mkopo wa fedha bila riba na itaendelea kutumia rasilimali za ndani kuwawekea wajasiriamali hasa wanawake ili kuendelea kiuchumi.

Sambamba na hilo, aliwataka wanaume kuwa na ushirikiano na wanawake katika harakati za maendeleo ikiwamo nafasi za uongozi lakini wanawake kutokubali kurubuniwa na wanaume hasa wanapogombea nafasi za uongozi.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema kuna changamoto zinazowakabili wanawake katika nafasi za uongozi ikiwamo kutojiamini na kuwa na kipato kidogo ikizingatiwa kuwa uchaguzi ni gharama.

Alisema wanawake wengi hushindwa kugombea nafasi za uongozi kutokana na uhaba wa fedha kwa sababu fedha huhitajika katika uendeshaji wa kampeni za uchaguzi.

"Wanawake kutokuwa na mafunzo ya kutosha ya uongozi pamoja na kutojiamini nazo ni miongoni mwa changamoto zinazowakabili wanawake kutofikia usawa wa kijinsia," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi (wapilikulia), akionyeshwa mchoro wa eneo litakalojengwa viwanda katika Kijiji cha PangaTupu, wakati wa ziara ya Wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Fedha UVIKO- 19 Kutekeleza miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali imeamua kuzitumia fedha za kupunguza makali ya Corona zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) katika miradi ya kijamii.

Amesema wananchi wa Zanzibar wanahitaji zaidi huduma hizo na kukamilika kwa miradi hiyo kutawapunguzia kufuata huduma muhimu kama elimu na afya masafa marefu.

Hemed aliyasema hayo jana alipotembelea na kukagua ujenzi wa miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema kuwapo kwa miradi hiyo kutatoa nafasi kwa serikali kusogeza huduma za kijamii, ikiwamo miundombinu ya barabara, maji na umeme ili kuwarahisishia wananchi wanaofika kupata huduma katika maeneo hayo.

Makamu wa Rais aliwaomba makandarasi wanaosimamia miradi hiyo kutoa fursa kwa wananchi wa maeneo hayo kwa kuwapatia ajira za muda ili wanufaike na miradi hiyo.

Kuhusu maeneo yanayopita miundombinu, alizitaka mamlaka husika kutoa nafasi kwa wakandarasi kuendelea na ujenzi wa miradi hiyo.

Hemed pia alizitaka wizara husika zilizopata miradi kuhakikisha wanasimamia fedha hizo na kuhakikisha malengo ya fedha hizo yanatimia na kuwakabidhi makandarasi wa miradi hiyo ili kuanza haraka kwa ujenzi.

Makamu wa Pili alisema serikali imeshatoa maelekezo kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya tathmini juu ya maombi ya wataalamu wa wizara hizo.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhamed Said, alimshukuru Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuelekeza fedha hizo katika miradi ya kujenga na kukarabati shule.

Alisema hatua hiyo inawajengea imani wananchi kwa serikali yao na kumhakikishia kuwa miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kuendelea na miradi mingine iliyopangwa na serikali.

Hemed pia alikagua ujenzi wa hospitali za wilaya ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi zilizoko Mwanakwerekwe, Chumbuni na Mbuzini, ujenzi wa hospitali ya mkoa Lumumba, ujenzi wa Shule ya Mwanakwerekwe D na G, Shule ya Sekondari Mtopepo na ujenzi wa madarasa ya shule ya Masingini.

# Wataka kamati za shule kujengewa uwezo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa Elimu Zanzibar, wameishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzipa nguvu kamati za wazee za shule ili kuzisimamia vyema na kuleta maendeleo katika shule.

Wadau hao waliyasema hayo jana wakati wakichangia rasimu ya Mwongozo wa Kamati za Shule katika ukumbi wa Kituo cha Walimu Kiembesamaki, mjini Unguja.

Mmoja wa wadau hao, Mmanga Omar Dadi, alisema ni vyema kamati za wazee zikapewa mamlaka ya kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara moja kwa moja ili kuzungumza nae kujua changamoto na maendeleo ya shule.

Alisema kuna changamoto katika kamati za shule zikiwamo wakusanyaji wengi wa fedha za mapato kutozifikisha sehemu husika.

Pia walisema kikwazo kingine ni baadhi ya walimu wakuu kutokuwa wawazi katika kamati kuhusu takwimu sahihi za walimu pamoja na kutotoa ripoti sahihi za ukaguzi wa shule.

Akiwasilisha rasimu ya marekebisho ya mwongozo wa kamati za shule, Mkuu wa Divisheni ya Sera katika Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Othman Omar Othman, alisema kuna haja ya kufanya marekebisho ya mwngozo huo ili uendane na wakati uliopo.


Othman alisema mwongozo uliopo ulikuwa umelenga zaidi katika malengo ya mwaka 2020 lakini wa sasa wanalenga kuelekea katika malengo ya 2050.

Alisema kumejitokeza mabadiliko mbalimbali ambayo yamefanya mwongozo huo wa zamani kutokidhi mahitaji, hivyo kuamua kuufanyia marekebisho.

Alitaja baadhi ya mabadiliko hayo kuwa ni pamoja na dira ya maendeleo ya Zanzibar ya 2050, malengo ya maendeleo endelevu (SDG), mfumo wa ugatuzi kufutwa pamoja na kufutwa michango ya wazazi au walezi katika elimu.

Akifungua mkutano huo, Ofisa Elimu na Mafunzo ya Amali Mkoa wa Kusini Unguja, Mohammed Haji Ramadhan, aliwataka wadau hao kuhakikisha wanatoa michango yao ili kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Naye Ofisa Mwandamizi wa Mradi wa Kukuza Ubora wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (EQSSEZ), Hassan Juma Hassan, alisema mradi huo unalenga kutoa mafunzo kwa walimu, kusaidia vituo vya walimu vifaa na kuihamasisha jamii kushiriki katika kukuza maendeleo ya elimu.



ZUCHU

UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI JANUARI 29, 2022



# ANAYEFUATA NI RAYVANNY?
## Kidogo kidogo moshi umeanza kufuka

JOTO linazidi kupanda kwa mashabiki wa muziki kutoka lebo ya WCB baada ya kutofahamu nani ameamua kujiengua, baada ya Harmonize kufanya hivyo miaka miwili iliyopita.

Kitendo cha Harmonize kuamua kujitoa WBC, hali ya hewa ilibadilika kiasi ambacho msanii huyo na aliyekuwa bosi wake Diamond Platnumz, kuwa katika vita kubwa iliyoambatana na majibizano ya maneno.

Lakini haijafahamika ni nani anayefuata baada ya Harmonize, lakini idadi kubwa ya mashabiki wana wasiwasi na Rayvanny kwamba ndiye aliyetabiriwa.

Wakati akitambulisha kundi jipya la Yamoto Band, Mkubwa Fela, alisema kwa kifupi kuwa yupo anayetaka kuondoka kitu ambacho alimuuliza Diamond, kama naye anamdai.

"Nilimwambia Diamond huyu anaondoka kakudhulumu? Akanijibu muziki wa Bongo Fleva nishaujua" amesema Fela.

Kila kiashiria kinamwangukia Rayvanny kwani licha ya kujiandaa kwa kuanzisha lebo yake ya muziki, pia kulikuwa na fununu kwamba ndiye alikuwa msanii wa kwanza kufikiria kuondoka.

Hata hivyo, Harmonize alijikuta akitangulia, labda kutokana na kukorogana na bosi wake kitu ambacho kilimfanya kukimbia haraka ili yasije yakamfika mabaya endapo angeng'ang'ani kubaki.

Mashabiki na wapenzi wa muziki wanasubiri kufahamu nani anafuata kufunga mlango wa WCB na kisha kwenda kuanza maisha sehemu nyingine.

## BASI SAWA

## Meja Kunta atoa siri nzito



MWANAMUZIKI wa singeli Meja Kunta, amekumbuka sakata la kujiua yeye mwenyewe akisema kilikuwa kipindi kigumu hadi akatamani kuacha muziki.

Akizungumza wakati akizindua EP yake yenye nyimbo nne, amesema baada ya kutoa taarifa hiyo ya uongo, wezi walivamia nyumba yake na kuiba kila kitu.

"Taarifa ile ilinipatia mitihani ya kuibiwa kila kitu, ilibidi nilale hotelini kiasi ambacho nilikata tamaa na kufikiria kuacha muziki kutokana na kuchoshwa kiakili," amesema Meja Kunta.

## Wengi wahuzunika kifo cha Artuk Bey



WAPENZI na mashabiki wa tamthilia kutoka Uturuki ya Ertugrul, wamekumbwa na huzuni kubwa kufuatia taarifa ya kufariki kwa Ayberk Pekcan, ambaye amecheza kama Artuk Bey.

Ayberk (51) ambaye amecheza kiustadi amekuwa akisumbuliwa na kansa kwa miezi kadhaa na taarifa ya kicho chake zimetolewa siku ya Jumatatu.

Nyota huyo amekuwa kipenzi cha mamilioni ya mashabiki ambao wanafuatilia tamthilia ya Ertugrul akiwa ni miongoni mwa wahusika wakuu.

Awali mwigizaji huyo aliwahi kuandika maelezo mafupi kuhusiana na hali yake ya kiafya miezi michache iliyopita kabla ya kifo chake akisema baada ya kufanyiwa uchunguzi ilibainika ana saratani ya mapafu na ilienea sehemu kubwa ya mwili.



# Zuchu azimika kwa Wamasai hawa

WIMBO mpya wa msanii Zuchu 'Mwambieni' umezidi kuwashika mashabiki kiasi ambacho kila kukicha watu wanatoa video za kuurudia kwa mitindo mbalimbali.

Hata hivyo, video iliyofanywa na Kili na dada yake Neema ambao ni Wamasai, imepata umaarufu katika mtandao wa Yiktok kiasi ambacho Zuchu ilimbidi kutoa neno.

"Nawapenda kwa kweli kwa sababu wameonyesha utofauti wa kupendeza kwa kuwakilisha utamaduni wetu," amesema Zuchu katika ukurasa wake wa Instagram.



# Profesa Jay azidi kuombewa

HALI ya mwanamuziki mkongwe wa Bongo Fleva, Profesa Jay imeelezwa si nzuri na anaendelea kupata matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili jijini Dar es Salaam.

Tangu kusambaa kwa taarifa hiyo, baadhi ya wasanii wamejitokeza kumpa pole, huku wakimuombea kwa Mungu amponye haraka na arudi katika shughuli zake.

Shilole katika ukurasa wake wa Instagram, ameandika kuwa kila wakati anamuomba Mungu azidi kumpatia nafuu ya haraka na kwamba anamsubiri jukwaani tena.

## Kono la Jini: Akumulikaye mchana, usiku anakuchoma

**Na Adam Fungamwango**

AKUMULIKAYE mchana usiku atakuchoma. Ni msemo wa kiswahili kuwa mtu anaweza kwa macho ya kawaida akaonekana ni mwema. Akakupa kila aina ya msaada unaouhitaji, lakini kumbe kwa upande wa pili si mtu mwema. Inawezekana huyo huyo ndiye akawa anakuumiza, halafu ukipata matatizo anakupa msaada, lakini nia yake ni kwamba akudhoofishe taratibu.

Ndiyo maana binadamu wenye roho ngumu wakiwemo wana usalama, yaani mashushushu na wapelelezi wao wana msemo wao kuwa 'usimuamini mtu yoyote hata kama akiwa maiti.'

Yaani kila kitu hata kama ni kizuri, au mtu mwema, usimuamini kwa asilimia mia moja.

Ni kwa sababu hata nchi kubwa kuna msemo kuwa hakuna rafiki wa kudumu au adui wa kudumu bali kuna masilahi ya kudumu. Rafiki wa leo anaweza kuwa adui wa kesho.

Tuiangalie filamu ya 'Kono la Jini'. Inashabihiana na hiki.

Inaanza mwanamke mmoja Kashinde kumtembelea shoga yake Mamu. Mumewe Mamu atatoka na kumtimua kwa kumtuhumu ni mchawi. Kitendo kile kinamkera mno mkewe kwani si mara ya kwanza kuwatuhumu baadhi ya majirani, lakini pia amekuwa na tabia ya kujitenga mno.

Tabia hiyo akaenda kuisema kwa rafiki na ndugu za mume, akitishia kuwa akiendelea na tabia hiyo, atadai talaka yake ya kuondoka.

Mamu akaenda kumueleza shoga yake mwingine tabia ya mumewe kupenda kukasirika bila sababu kuongea peke yake kama ana mapepo. Shoga yake akampa dawa amuwekee kwenye chai. Omari ambaye ndiye mume wa Mamu anashtukia hakunywa. Badala yake anamfokea mkewe na kusema naye amejiunga kwenye kundi la watu wabaya. Omari anaamua kuhama na mkewe. Mke anamuuliza, lakini mume anamwambia yeye ndiye ameamua.

Siku moja mkewe alishuhudia kwa macho yake mumewe alitokewa na mkono



wa ajabu, unajipachika kwenye mkono halisi. Kitendo hicho kinamfanya kuogopa mno, lakini anajipa ujasiri anaamua kumuuliza baada ya mkono huo kutolewa. Omari anaambiwa alipewa nguvu hizo na babu yake na ndizo zinamfanya kutambua wachawi, ambao wanataka kumuua, lakini wameshindwa. Nguvu alizopewa zinaitwa mkono wa jini ambao humtokea na kutoweka kila baada ya muda na ndiyo maana kuna wakati anakuwa anajitenga.

Kumbe wakati wote huo kulikuwa na vita kubwa kwa wachawi wa kijiji kile kutaka kumuua Omari kutokana na kuonea kijicho kwa nguvu alizonazo za mkono wa jini. Lakini wamekuwa wakimshindwa kutokana na nguvu hizo hizo.

Omari anamwambia mkewe kutokana na nguvu na mkono wake leo atawaona wachawi wote wanaomsakama. Mamu akawaona. Akaamini.

# KAMBA ZA MIDUME ENZI HIZO

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE mapenzi wakati mwingine kuna uongo mwingi sana. Hutumika kushawishi au kukufanya uheshimike na kukubalika. Siku zote uongo una mwisho wake. Ukweli unapobainika ndipo matatizo mengi yanapokuja.

Wanamuziki wa zamani wametunga nyimbo nyingi sana zenye maudhui ya uongo kwenye mapenzi na hata ndoa.

Leo tutaangalia nyimbo ambazo wanaume 'wamewapiga kamba' wanawake ili wawapate, au kuwashawishi wawaache waume zao.

**KARUBANDIKA-MAQUIZ ORIGINAL**

Huu ni wimbo maarufu sana. Ulitungwa na marehemu Kasaloo Kyanga akiwa na Maquiz Original, katikati ya miaka ya 1980. Unamuonyesha mwanadada akilalamika juu ya uongo aliopewa na kijana Karubandika. Ni kwa bahati nzuri tu, dada alishtuka mapema.

Jamaa huyu alipenda demu, lakini badala ya kumwambia ukweli akamdanganya kama ni mkurugenzi wa kampuni fulani. Ukweli ni kwamba jamaa kazi hana, analala kwenye stendi ya basi. Demu alishtuka na urafiki ukaishia hapo hapo.

**PENDO-BIMA LEE**

Hapa sasa jamaa anajisifia uongo. Anamwambia mpenzi wake baada ya kumuongopea kumtoa kijijini na kuleta mjini kuwa ni meneja na ana miradi mbalimbali, ikiwemo ufugaji, kumbe kamba tu.

Anamwambia laivu mpenzi wake kuwa tangu enzi za mababu, mwanaume akimpenda mwanamke, eti uongo ni lazima usemwe japo kidogo.

Hii ni baada ya mwanaume kumlalamikia kwa nini alimtoa kijiji kwa kumdanganya kiasi hicho kumbe hana lolote huku mjini. Jamaa anamwambia alimdanganya kwa sababu anampenda.

Ulitungwa na marehemu Jerry Nashon 'Dudumizi' akiwa na bendi ya Bime Lee mwishoni mwa miaka ya 1980.

**KALUMANZIRA-JUWATA JAZZ**

Nao huu pia ni wimbo wa katikati ya miaka ya 1980. Unaitwa 'Karumanzira', wa bendi ya Juwata Jazz 'Msondo Ngoma', utunzi wake marehemu Said Mabera. Ni mwanadada anayelalamika kudanganywa na Karumanzira kuwa amuache mumewe, ili amuoe yeye. Awali dada huyo hakukubali kitu hicho. Lakini kwa bahati mbaya baadaye aliachika, siyo kwa ajili ya Karumanzira. Baada ya kuachwa akamkumbuka jamaa huyo aliyesema atamuoa. Akamfuata, jamaa akawa anampiga chenga kwa miaka miwili, akionekana kabisa hataki kumuoa kama alivyokuwa akimwambia huko nyuma.

**HOMA IMENIZIDIA-OSS NDEKULE**

Wimbo huu hautofautiani ya ule wa 'Karumanzira'. Umetungwa na Hassan Rehani Bitchuka akiwa na bendi ya Orchestra Safari Sound na mtindo wao wa Ndekule wakati huo, katikati ya miaka ya 1980.

Mwanamke analalamika kudanganywa amuache mumewe ili akaolewe na mwanaume mwingine aitwaye Rehani, lakini alipofika huko, akaishi kipindi kifupi tu, akatimuliwa, kisa eti hana tabia nzuri.

Dada huyo anawaasa wanawake walioolewa wajihadhari na wadanganyifu, kwani wakiachana waume zao watapotea.

**MAYANGA-MAQUIZ ORIGINAL**

Mayanga pia ni mwanaume mwongo. Huyu alimpata demu Sumbawanga, akamleta mjini akimdanganya kuwa ni meneja, lakini kumbe siyo. Sasa mambo yamechacha. Kumbe alikuwa na pesa za muda tu, sasa nyumba imepigwa mnada sababu ya madeni, fenicha zimechukuliwa, kila kitu ni tatizo, mpaka mwanamke anamshauri bora warudi wote Sumbawanga wakaanzishe maisha mapya.

Wimbo huu ulipigwa na Maquiz Original mwanzoni mwa miaka ya 1990.

# Okposo hukujua mchepuko hauna dili?



MWANAMUZIKI wa injili wa Nigeria, Sammie Okposo, amemuomba radhi mke wake hadharani kutokana na kuibuka kashfa ya kutoka nje ya ndoa yake.

Okposo ambaye ni maarufu kwa uimbaji wa nyimbo hizo za kumsifu Mungu, amemuomba radhi mkewe Ozioma kupitia ukurasa wake wa Instagram na baada ya saa chache alifuta.

"Mke wangu  Ozioma, kwa heshima nakuomba radhi kutokana na aibu hii iliyokupa usumbufu. Nimeuvunja moyo wako na uaminifu. Nisamehe kwa kukuangusha na kukupatia maumivu," aliandika Okposo.

Hivi karibuni mwanamke mmoja aliyejitambulisha kama African Doll, amesema amekuwa na uhusiano wa kimapenzi na msanii huyo wakati walipokuwa Marekani akifanya ziara yake ya muziki.



## Card B ajizolea bilioni 1.9 kama masihara

RAPA mwenye utata wa Marekani,Cardi B, amelamba dola milioni 1.25 kama fidia baada ya kushinda kesi ambayo alishtaki mtandao mmoja kwa kumchafulia jina lake.

Card B alimshtaki mwanablogu huyo kwa kukashifu, kuingilia faragha yake kwa kumuita kama mgonjwa wa malengelenge, mtumiaji wa dawa ya kulevya na alifanya kazi ya ukahaba.


Katika ripoti ya Billboard, Mahakama ya Georgia ilimpa kiasi hicho sawa na shilingi bilioni 1.9, baada ya wiki mbili za mashauriano.

## Priyanka kawa mama

BAADA ya kelele nyingi kutoka kwa mashabiki wao, hatimaye mwigizaji kutoka Bollyhood, Priyanka Chpra na mwanamuziki wa Marekani, Nick Jonas, wametangaza kumpata mtoto wao wa kwanza.

Mrembo huyo wa Dunia, kupitia ukurasa wake wa Instagram amemkaribisha mtoto kwa kuelezea yeye na Jonas wana furaha kwa kuongeza familia yao.

Priyanka na Nick walianza uhusiano wa kimapenzi mwanzoni mwa 2018, na ilipofika Desemba walifunga ndoa.





## Filamu ya Kanye, Kim yazidi kunoga

WATU wanasaka kwa kila hali video ya ngono ya Kim Kardashian na Ray J, lakini wasichokijua kuwa pengine imekuwa janja ya Kanye West, kujiimarisha.

Kanye wakati akihojiwa huko HYPERLINK "https://www.youtube.com/watch?v=OqkgyU-Tu84" Hollywood, alidai ameifuma video hiyo katika kompyuta mpakato ya Ray na kisha yeye alimtumia Kim na kumsababishia kuangua kilio.

Hata hivyo, msemaji wa Kim amesema bosi wake alilia kwa furaha baada ya Kanye kumpelekea kompyuta hiyo ikiwa na picha za kumbukumbu za safari yao nchini Mexico, hivyo hakukuwepo na video kama hiyo.

## Macaulay wa 'Home Alone' apata mchumba

MWIGIZAJI maarufu wa filamu za Home Alone, Macaulay Culkin hatimaye amevunja ukimya baada ya kutangaza kumchumbia mpenzi wake wa siku nyingi Brenda Song.

Kulingana na jarida la People, nyota huyo alizungumza na mama yake kuhusu maandalizi ya mtoto watakayempata akiwa na mke wake huyo mtarajiwa.

Awali, Song alionyesha pete ya madini ya dhahabu ambayo ameivaa kwenye kidole chake wakati alipotua katika mgahawa mmoja eneo la Beverly Hills.



MAKALA

## UHURU KUTUMIA TV, REDIONI...

# Taifa linavyofanikisha wito wa haki ya vijana wakipishana na magumu

**Na Rajabu Msangi,** SJMC

## •Ombi la UNICEF& UNESCO 2015




Watu wakiwa katika mkusanyiko kufuatilia matangazo ya runinga , wengi wao vijana. **PICHA: MTANDAO.**

"Mwenye macho haambiwi tazama,"ndivyo waswahili wanavyosema, japokuwa sio kila kitu kinapaswa kutazamwa. Uwepo wa sayansi na teknolojia umeibua mengi ambayo baadhi yake hayapaswi kutazamwa na mtoto hasa yanayooneshwa katika vyombo vya habari ikiwamo televisheni.

Mtoto kwa mujibu wa Sheria ya Watoto nchini, inamtambua kuwa mtu mwenye umri chini ya miaka 18. Katika nafasi yake ana haki anazostahili kupatiwa, ikiwamo kulindwa, kupewa elimu, kucheza, kuishi na hata haki ya kupewa Uhuru wa kujieleza, ambazo pia katiba ya nchi inaieleza vyema.

Kiuhalisia, haki ya elimu ni kama imepewa mgongo na jamii, pamoja na kwamba serikali inazidisha juhudi zake kuhakikisha mtoto anapata haki ya elimu tena bure pasipo malipo. Pia, vyombo vyombo vya habari vimekuwa na taswira chanya kwenye taaluma za watoto.

Kupitia vyombo hivyo kama vile radio na televisheni vimekuwa na mchango mkubwa katika elimu yao, hasa kupitia vipindi vinavyoandaliwa mahususi kwa ajili yao

**FANI NA TAALUMA**

Katika ujumbe wake kwa mwaka 2015 uliotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi, Elimu na Utamaduni UNESCO, lilitoa wito wa kushirikisha zaidi vijana katika vyombo vya habari.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa UNESCO, Irina Bokova anasema mara nyingi vijana wa kike na kiume wenye umri wa chini ya miaka 30 hutengwa katika kuandaa na kutangaza vipindi vya radio na kwa mantiki hiyo, akavisihi vyombo vya habari na hasa redio kuwapa vijana nafasi ya kujieleza.

Nchini Tanzania hilo limepokewa na kuanza kutendeka na mtandao wa wanahabari watoto, ambao, kupitia usaidizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia watoto, UNICEF , unahamasisha watoto kujifunza utalaamu wa kutengeneza taarifa na vipindi mbalimbali vya redio, hivyo kupata nafasi ya kuzungumzia kinachowagusa zaidi.

**WAHUSIKA WAONGEA**

Mariam Daudi ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Ubungo Kisiwani, Dar es Salaam, anasema mbali na masomo wanayoyapata darasani, pia kuna baadhi ya vipindi vinawaelimisha sana kupitia televisheni.

"Kuna baadhi ya vipindi vinatufundisha kuwa na maadili mema, pia kujifunza masomo kama vile hesabu kwa mfano katika kipindi cha Akili na Ubongo Kids," anafafanua.

Mtoto Lukman Adam, mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Ubongo Kisiwani, anasema hawaishii kujifunza vya darasani pekee, bali hata maadili na mengine katika jamii wanayojifunza kupitia vyombo vya habari.

"Hata katika tamthiliya tunazoziangalia tunavyokuwa nyumbani, tunajifunza kuwa na heshima kwa wazazi wawili, kuwa na upendo kwa marafiki zetu na hata kujiepusha na mambo mabaya kama vile wizi na hata kutumia dawa za kulevya," anasema.

**MAJIBU YA UPOTOSHAJI**

Inaelezwa wengi katika umma wamekuwa na dhana hasi juu ya vyombo vya habari mfano televisheni, dhidi ya malezi ya watoto. Hiyo inatokana na maudhui yanayoonyeshwa katika baadhi ya vipindi. Hapo swali la kujiuliza, ni aina gani ya kipindi ambacho mtoto anafaa kutazama. Pia, maudhui ya aina gani?

Baada ya kufumbua majibu ya maswali hayo, ndiyo imetoa njia pekee ya kutambua athari zinazopatikana katika vyombo vya habari na watoto.

Msimamizi na Mhariri wa Mlimani Tv Silvano Kayera, anasema mbali na kujali vipindi vinavyobeba uhalisia kwa jamii, pia Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) imetoa maelekezo kwa waandaaji wa vipindi kulenga pia maudhui yatakayotoa elimu kwa watoto.

Kwa upande wa maudhui ambayo hayana maarifa kwa watoto, Kayera anatoa wito kwa waandaaji wa vipindi kuangalia maudhui yanayojenga taaluma za watoto, pia kuwepo ushirikiano wa wazazi katika kupanga muda sahihi wa watoto kutazama televisheni.

"Kwa kuwa tunaamini vipindi vinavyoonyeshwa kwenye tv na redio vinawagusa watu wa rika zote ikiwemo watoto, kuna baadhi ya maudhui sio rafiki katika kujenga maarifa ya mtoto, hivyo kunatakiwa kuwe na ushirikiano mkubwa kwa mzazi kujua ni aina gani ya kipindi ambacho mtoto anapaswa kutazamwa na vipi hapaswi kutazama."

Kutanda kwa hali hiyo imepelekea baadhi ya wazazi kuwakanya watoto wao hata kutazama televisheni kwa vipindi ambavyo ni mahususi yanayowahusu, wakidhani maudhui ya vipindi yanaharibu tabia kwa watoto.

Mwanafalsafa wa nchini Uhispania, George Santayana ameshawahi kuanika mtazamo kuwa: "Mtoto aliyefundishwa shuleni tu ni mtoto asiyejifunza."

Kuna wakati mtoto anatajwa anaweza kupata maarifa kutokana na maudhui yanayorushwa katika vipindi vya runinga.

Nchi ya Tanzania kuna bahati ya kuwa na idadi kubwa ya watoto katika maeneo mbalimbali ambao wengi wao, elimu kubwa wanayoipata shuleni imekuwa ikiwatosheleza hasa ikizingatia masalahi ya wakazi wa vijijini.

Kisaikolojia, mtoto ana uwezo wa kunukuu kila kinachotendeka na kuonekana katika vipindi vya televisheni.

Pia, baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwaachia uhuru watoto wao kutazama televisheni bila kujali ni maudhui yanayoonyeshwa kwa muda huo. Ni namna inayochangia kuharibika tabia za watoto wangali bado wadogo.

Bwelela Msangi ni mkazi wa Ubungo River Side, mzazi wa watoto watatu ametoa wito kwa waandaaji vipindi kulenga vipindi ambavyo vitakuwa na tija kwa watoto hao.

"Sisi kama wazazi sio kwamba tunawakataza watoto kuangalia televisheni, lakini kuna wakati kama mzazi umekaa na watoto lakini baadhi ya vipindi havina maudhui mazuri kwa watoto.

"Hata muziki ambao umekuwa ukionyeshwa kwenye runinga, picha zake hazina utamaduni ukizingatia mavazi wanayovaa hasa kinadada ambao mara nyingi hufanya hivyo," anaeleza

Kuna wakati mbali na uangalizi sahihi wa wazazi katika malezi, watoto wana ubunifu mkubwa katika akili zao na hata wengine kuwa na vipaji vikubwa pasipo kujua. Hapo wengine wanajifunza kupitia vipindi vya watoto, ambavyo vimekuwa vikionyeshwa katika runinga mahususi kwa ajil yao.

Watoto wanaotambuliwa kuwa Taifa la Kesho, kuna seali juu yao kwanini wasilelewe kwa usahihi?

Hjapo inaibua wajibu wa kijamii kutambua umuhimu wa kutazama vipindi vyenye maudhui ya watoto katika kukuza taaluma zao na maarifa sahihi yenye uadilifu katika jamii.

Kwa ujumla vyombo vya habari vina majukumu mengi kwa watoto ikiwamo kutoa elimu kwa wazazi na walimu juu ya haki na mahitaji muhimu kwa watoto. Aidha, vinawafunza watoto kuzijua haki zao, maisha, utamaduni na namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika maisha yao.

# Siri hadi ikapewa jina la 'Kaunda Suti' vazi lenye mzizi tangu 1920

Na Adam Fungamwango

SUTI ni vazi linalompendeza na kumheshimisha mtu yoyote anayelivaa, kuanzia waheshimiwa hadi 'masela' mtaani.

Hata mhuni akivaa suti, na akienda ambako hajulikani watamheshimu na kumpa kipaumbele kwa kitu chochote anachohitaji, bila kujua hayuko kama wanavyodhani.

Hata watu wanaotaka kwenda ukweni kwa mara ya kwanza, mara nyingi wanakwenda na suti hata kama ya kuazima.

Lengo ni kutaka waheshimike hasa kwenye hatua za mwanzo na kukubalika ukweni, haijalishi kama baadaye wataonekana hawana lolote.

Vazi la suti lina heshima yake, kiasi kwamba hata mitaani watu wamelitungia kanuni, ingawa si rasmi.

Wanasema ukivaa suti kwanza kabisa usipande daladala, bajaji wala bodaboda, badala yake lazima uwe na gari lako au ukodishe taxi.

Pili usiingie kwenye vibanda vya mama lishe kula chakula, badala yake mvaa suti ni lazima aingie hotelini.

Tatu ukivaa suti ni lazima uepuke kununua vitu vidogo vidogo njiani kama hindi la kuchoma, karanga na chochote kinachofanana na hicho.

Wapo walioenda mbali sana eti hata ukiporwa pesa na kibaka usimkimbize, kwani utashusha hadhi ya vazi hilo.

Kama nilivyosema ingawa hii siyo sheria, lakini watu wanasema hivi kutokana na kuliheshimu vazi hilo. Ukweli ni vazi linaloheshimiwa sana, si Tanzania tu, bali duniani kote.

Hata hivyo kuna aina tofauti za suti. Kuna suti ambazo wanavalia tai. Kuna aina nyingine ambayo ilikuwa kama vazi rasmi la Rais wa zamani wa Zambia, Kenneth Kaunda kiasi cha kupachikwa jina likaitwa 'Kaunda Suti.' Yenyewe ina aina yake ya utengenezaji na pia haivaliwi na tai.

Aina hii ya suti hapa nchini Tanzania imekuwa maarufu sana kwa sababu inavaliwa na wabunge, baadhi ya mawaziri, na maafisa mbalimbali wa serikali na idara zake zote, kiasi cha kuonekana kama ni vazi lao rasmi.

Vazi hilo ndiyo lilikuwa 'pamba' za mzee Kaunda aliyefariki Juni 17 mwaka jana, na alilivaa wakati wote, baada ya kuingia madarakani, akiwa madarakani na hata alipoondoka.

Kupenda kwake kuvaa vazi hilo, ndiyo watu wakaamua kulipa jina lake, wakaliita 'Kaunda suti.'

Je awali kabla ya kuanza kuvaa mzee Kaunda halikuwepo? Na kama lilikuwepo liliitwaje?



Awali suti hizo ziliitwa 'Safari suti'.

Zilibuniwa miaka ya 1920 na Wafaransa wawili Ted Lapidus na Yves Saint Laurent ambao walikuwa ni wabunifu wa mavazi na wanamitindo.

Lengo lilikuwa ni kubuni suti za kusafiria kutoka nchi zenye baridi Ulaya kwenda nchi za joto Afrika. Zilitengenezwa kwa pamba na haikuwa na haja ya tai. Wao wazungu waliona tai ni kwa nchi za baridi tu na si Afrika.

Hapa kwa mbali, nataka kuanza kuwaamini wale jamaa wanaodai ukivaa suti ni lazima uwe na gari lako na si kutembea kwa miguu umbali mrefu, kwa sababu ya joto si Bongo tu, bali Afrika.

Hawa nadhani walimaanisha zile suti za tai na ndizo zenye masharti mengi yaliyowekwa kwa watoto wa mjini.

Inawezekana suluhisho la yote hilo ni kuvaa kaunda suti ambazo hata wazungu wenyewe kumbe walizitengeneza kwa matumizi ya hali ya hewa ya joto Afrika.

Si yeye tu, kuna baadhi ya viongozi nao walikuwa wanapenda kuvaa mavazi na kuvuma, kama Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania akivaa kama waasisi wa Ukomonisti nchini China

Mao Tse Tung na Chou en Lai, ambayo ni suti isiyo na kola, Wabongo wakibatiza jina la 'Chunlai', Rais kwa kwanza wa Ghana, Kwame Nkurumah akivaa vazi lililoonekana kama mgolole hivi na Rais wa wakati huo wa Congo Brazaville Marien Ngoabi, naye alikuwa na aina yake ya suti, Wabongo wakaiita 'Ngwabi', lakini wote hao walifunikwa na Kaunda.

Tangu wakati huo hadi leo hii, wanamitindo, wabunifu wa mavazi na hata mafundi cherehani na maduka ya nguo dunia nzima, wanapoweka matangazo ya biashara zao, vazi hilo wanaliita jina la rais huyo, yaani 'Kaunda suti'.

**KAUNDA ALIITAWALA NCHI HIYO**

kwa miaka 27 hadi Novemba 2 mwaka 1991, alipoangushwa kwenye uchaguzi.

Anachukuliwa kama mmoja wa mashujaa wachache walioshiriki kuikomboa Afrika, chini ya, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hata hivyo mwaka 1991, baada ya yeye na chama chake cha UNIP kuangushwa na kuingia madarakani Fredrick Chiluba, kulitokea maasi na kutaka kumpindua rais huyo mwaka 1997.

Kutokana na hali hiyo Chiluba, akamtia mbaroni mzee Kaunda, wakati huo akiwa na miaka 73, akimtuhumu kushirikiana na watu waliokuwa wakitaka kumpindua.

Dunia nzima ilishtuka, na rafiki yake kipenzi, Nyerere alilazimika kwenda nchini Zambia na kuokoa jahazi. Alifika nchini humo na kwenda kwenye gereza lililokuwa maeneo ya Kabwe.

Nyerere aliingia ndani ya gereza hilo hadi sehemu ambayo Kaunda aliwekwa, akala naye chakula. Akazungumza naye kiasi cha saa mbili hivi na kitu, akatoka.

Baada ya muda, Rais Chiluba akatangaza kumfungulia mzee Kaunda.



HABARI KIMATAIFA

# Marekani, China zashindana kuifikia ndege ya kijeshi iliyoanguka baharini

**WASHINGTON,** MAREKANI

USHINDANI mkubwa umeibuka kati ya majeshi ya Marekani na China, kuifikia ndege ya kivita iliyoanguka wakati wa mazoezi ya kijeshi.

Ndege hiyo ya F35-C ya Marekani, ilianguka Kusini mwa bahari ya China baada ya kile Jeshi la wanamaji la Marekani linaelezea kama ni tukio la bahati mbaya wakati ilipokuwa ikipaa kutoka kwenye meli inayobeba ndege za kijeshi ya Marekani USS Carl Vinson.

Ndege hiyo ya kivita ndiyo mpya zaidi katika Jeshi la Wanamaji la Marekani, na imejaa vifaa vya kisasa na kusababisha kila nchi kukimbilia eneo la tukio kuiokoa ndege hiyo.

Wanamaji saba walijeruhiwa wakati ndege hiyo ilipoanguka siku ya Jumatatu baada ya kugonga eneo moja la meli ya Vinson wakati wa mazoezi ya kijeshi.

Kwa sasa ipo chini ya bahari, lakini kinachotokea ni siri kubwa kwa Jeshi la Marekani, hivyo limekataa kusema ni wapi ndege hiyo ilipoanguka na itachukua muda gani kuitoa majini.

China inadai umiliki wa karibu eneo lote la bahari ya kusini mwa taifa hilo, na imezidi kutoa madai hayo katika miaka ya hivi karibuni, ikikataa kutambua uamuzi wa mahakama ya kimataifa ya 2016 ambayo ilisema hauna msingi wa kisheria.

Wataalamu wa usalama wa taifa walisema jeshi la China litakuwa na hamu sana ya kuwa wa kwanza kuifikia ndege hiyo huku meli ya uokoaji ya Marekani ikionekana kuwa itachelewa siku 10 kutoka eneo la ajali.

Mshauri wa Abi Austen, alisema itakuwa imechelewa kwa sababu betri ya sanduku jeusi katika ndege hiyo itakufa kabla ya wakati huo, na hivyo kufanya kuwa vigumu kupata ndege.

"Ni muhimu sana Marekani kuifikia kwa haraka kwa sababu F-35 kimsingi ni kama kompyuta inayoruka. Imeundwa kuunganisha mashambulizi, " alisema.

Alipoulizwa kama kulikuwa na mwangwi wa vita baridi, alisema yote hayo yanatokana na nani mwenye uwezo mkubwa wa kijeshi.

Timu ya wasimamizi wa uokoaji kutoka jeshi la wanamaji la Marekani itapeleka mifuko kwenye kifusi hicho cha ndege ambayo itawekwa hewa ili kuweza kuja juu na kisha kuopoa majini na kuibeba ndege hiyo .

Ndege hiyo inaelekea ilikuwa na makombora kadhaa yaliyobebwa kwenye mabawa yake.

**BBC**



Wanamaji wa Marekani na Ufilipino wakifanya mazoezi katika bahari ya kusini mwa China **(PICHA: BBC)**

## Wahamiaji 6 wafa maji

**TUNIS,** TUNISIA

WAHAMIAJI sita wamekufa maji na wengine 30 hawajulikani waliko baada ya mashua waliyokuwa wamepanda kupinduka katika pwani ya Tunisia.

Watu 34 waliokolewa na wanamaji wa meli za walinzi wa pwani ya nchi hiyo.

Walionusurika walisema wahamiaji 70 walikuwa wamepanda mashua hiyo, kutoka mataifa mbalimbali yakiwemo Misri, Sudan na Morocco.

Msemaji wa jeshi la Tunisia, alisema wahamiaji hao waliondoka Libya na walikuwa na matumaini ya kwenda Ulaya.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi UNHCR linasema kuwa katika miezi tisa ya kwanza ya mwaka jana, wahamiaji wasiopungua 1,300 walitoweka au kufa maji wakijaribu kuvuka kutoka Afrika Kaskazini kuelekea Italia.

**BBC**

## Watu 6 wauawa vurugu Darfur

**NEWYORK,** MAREKANI

MACHAFUKO mapya ya kikabila katika eneo la Darfur nchini Sudan, yamesababisha watu tisa kupoteza maisha na wengine zaidi ya 15,000 kukimbia makazi yao katika kipindi cha wiki moja.

Kulingana na ripoti ya Umoja wa Mataifa, ilisema mzozo wa kibinafsi kati ya wanaume wawili kutoka kabila la Masalit na kundi la wahamaji wa Kiarabu ulisababisha kuibuka kwa vurugu karibu na mji wa El Geneina.

Wahamaji wenye silaha walishambulia soko la ndani, walichoma moto sehemu ya kijiji, na kuua watu tisa wakiwemo watoto wawili.

Mapigano hayo pia yalilazimisha zaidi ya watu 4,000 kutoroka kuvuka mpaka hadi Chad. Zaidi ya watu milioni mbili bado wanaishi katika kambi kutokana na mzozo wa Darfur wa mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Mwaka jana kulishuhudiwa ghasia tena huko Darfur na mashambulizi ya mara kwa mara kwenye kambi na vijiji kutoka kwa wanamgambo.**BBC**

# Museveni aonya wanaowakataa wanafunzi waliobeba mimba

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni amepinga uamuzi wa Askofu wa Kanisa la Katoliki kuwazuia wasichana wajawazito kurudi shuleni baada ya shule kufunguliwa mwezi huu nchini Uganda.

Kutokana na janga la Covid- 19 shule zilifungwa nchini humo kwa kipindi cha miaka miwili, na kusababisha wasichana wengi kupata ujauzito.

Askofu wa Dayosisi ya Mukono, James Ssebgala, aliwaamuru walimu wa shule zinazomilikiwa na Kanisa hilo zisiwaruhusu wanafunzi wajawazito kurudi shule baada ya shule kufunguliwa Januari 10, mwaka huu.

Askofu huyo alipinga mpango wa wizara ya elimu nchini humo wa kuwaruhusu wanafunzi wote waliobeba mimba na wale waliojifungua wakati wa zuio la kukaa nyumbani warudi shuleni kuendelea na masomo.

Aliwataka walimu kuwapeleka wanafunzi katika vituo vya afya wapimwe kabla ya kuanza masomo na yule atayepatikana na mimba wamrudishe nyumbani.Katika hotuba yake kwa taifa kuazimisha miaka 36 ya chama chake cha NRM kuingia madarakani , Rais Museveni alipinga agizo hilo la askofu.

"Kitu ambacho naweza kukwambia wazi nisichokubaliana nacho , ni kumlaumu msichana asiendelee na masomo kwa sababu alipata ujauzito kwa mara ya kwanza, siwezi kukubalina na hilo hata katika masuala ya kidini, kwa sababu mtoto kama alifanya makosa huwezi kumlaani katika maisha yake yote na kumkatisha masomo yake," alisema.

"Mbona kuna mama wazee zaidi ya miaka 50 wanarudi shuleni kusoma? kwanini umkatize mtoto masomo wakati alipata matatizo". Alihoji Rais Museveni.

Tangu shule zifunguliwe nchini Uganda takwimu za wizara ya elimu zilionyesha kati ya wanafunzi milioni 15 nchini kote, asilimia 30 hawajarudi shuleni kutokana na ujauzito na kujifungua.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**BOAZ THOMAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.2561-0009** iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari **SONGWA** mwaka **2011**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/608355/2021.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF MBINGA**
**DISTRICT AT MBINGA**
**MISC.CIVIL APPLICATION NO.16/2021**

**DAIB SALUM……….....................APPLICANT**
**VRS**
**SUCASTAINABILITY TANZANIA LTD…………1ST RESPONDENT**
**KILIMO KWANZA GROUP…………...................2ND RESPONDENT**
**SABRI DAIBU SALUM………3RD RESPONDENT**

**TO: SUCASTAINABILITY TANZANIA LTD**

**TAKE NOTICE:** That the above Misc. Civil Application has been set down for hearing on the 9th day of February 2022 at 08:00 in the forenoon thereafter.
You must produce on that day all the witnesses upon who evidence and all the document upon which you instead delay in support of your case.
GIVEN Under my hand and the SEAL of the court this 26th January 2022.

……………………
**DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE**
**MBINGA**
Place: MBINGA DISTRICT COURT
Copy to Respondent
Received copy of this notice

…………………………...
**RESPONDENT**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIZABETH JONATHAN KASIMILA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya Nissan X-Trail yenye namba za usajili **T684DJN**. Chassis No. **JN1TBNT30Z0106062,** Engine **No. QR25366390A.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi DOD/DOD/RB/38502/2022.

---

## TANGAZO!!
## AFRIWELD INDUSTRIES LTD
## Nafasi ya kazi

Wanahitajika wasichana Wenye umri kuanzia miaka 25-35
**Nafasi:** Mauzo
MSHAHARA wa kuvutia utatolewa!!
wahi sasa Kupata nafasi nzuri!!
Kwa mwasiliano zaidi piga simu namba: **0719 184 070**
Piga simu muda wa kazi TU saa MBILI mpaka saa KUMI NA MOJA jioni
01/01/2022 MPAKA 31/01/2022
**Asante**
116653602

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FREEDOM NELSON MANGA**
Anatanga kupotelewa na kadi ya gairi yenye namba za usajili **T.560 CWC** aina ya **MAZDA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi
**KAH/RB/71/2022.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF ILEMELA DISTRICT AT ILEMELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.19 OF 2021**
**In the matter of the Estate of the Late DEOGRATIAS TRIPHONE MASANJA**
**AND**
**In the matter of Application for Grant of Letter of Administration by HONORATI MICHAEL MASANJA.**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All person clamming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant for letters of probate and Administration is made to the above named petitioner Caveat/objection to the grant should be filed on or before 9TH day of **FEBRUARY, 2022.**
Dated at Mwanza this **19TH day of JANUARY, 2022.**

Dated at Mwanza this 19TH day of JANUARY, 2022.
RESIDENT MAGISTRATE
ILEMELA – MWANZA.

……………………………….
**RESIDENT MAGISTRATE**
**ILEMELA-MWANZA.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la MADAI NAMBARI 06/2021**

**Jina la Mdai IBRAHIM LUCAS VICENT**
**Jina la MDAIWA MARTHA PATRICK MALODA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
Kwa MARTHA PATRICK MALODA wa MBEYA 0659617173
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ya TALAKA
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 3/2/2022 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 27/01/2021

…………………………………………………
**HAKIMU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la MADAI NAMBARI 07/2021**
**Jina la Mdai LUSAJO SAIMON MWAKIBINGA**
**Jina la MDAIWA MARRY JONATHAN MBASHA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
Kwa Marry Jonathan Mbasha wa Geita 0752612914
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ya TALAKA
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 3/2/2022 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 27/01/2021

…………………………………………………
**HAKIMU**

---

## PLOT AND HOUSE FOR SALE-MTONI KIJICHI

PLOT AND HOUSE FOR SALE AT MTONI KIJICHI-TEMEKE DISTRICT SQUARE METER 6937. PLOT IS SUITABLE FOR ANY COMMERCIAL BUSINESS, OFFICE, RESIDENTIAL OR ANY KIND OF ESTABLISHMENT. PRICE IS NEGOTIABLE.
**CONTACT: 0659532007**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA .**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Mfaranyaki Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma.**
**Shauri la Rufaa Na.03,2021.**
**Shauri Asilia Jinai ,Madai**
**(ya Kawaida/Talaka) Mirathi Na.57,2021.**
**Jina RAMADHAN .G.MSUKU, muomba rufaa/Masahihisho ,Madai/Mdaiwa wa ,M/Mwanzo Dhidi ya AMINA .G.MSUKU ,Mjibu Rufaa /Masahihisho ,Madai /Mdaiwa wa M/Mwanzo kwa AMINA GABRIEL MSUKU .**

Fahamu kwamba Rufaa /Masahihisho itasikilizwa katika Mahakama hii Saa 08:30 asubuhi /mchana tarehe 23 mwezi 02 mwaka 2022 Hati hii imetolewa kwa amri ya Mahakama hii leo tarehe 26/01/2022 .

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**SONGEA.**
**(Wakili)**
Usikose kufika tarehe na saa katika Mahakama hapo juu.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SPANISH TILES AND SANITARY WARES LTD**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T140 DAK TOYOTA NOAH Engine No. 1AZ5280440. Chassis AZR600473142 na CC 1990.** Atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB/593691/2021.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**TWAIBA JUMA MINGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha **UALIMU** kozi ya **UALIMU WA ELIMU YA MSINGI-ASTASHAHADA** kilichotolewa na chuo cha **UALIMU VIKINDU** chenye registration namba **VTC/IIIA/2016/4128** mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/MBA/RB/25867/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**VELAILA STEPHANO MWIJAGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1577-0037** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FANAKA MEMORIAL SEKONDARI** mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PWA/MAP/RB/479291/2021.**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 06 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late BENARD SKAPH KILENDU**

**By 1.WINIFRIDA BENARD KILENDU**
**2. ……………………………..**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 07th day of FEB ………2022

**Dated at MOROGORO this 11 day of 01/2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KADI YA GARI

**YUSUPH SAID BABU ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI(STATION WAGON) yenye namba za usajili T 177 CWT Chassis namba: ACM265010614 Injini namba : 2AZ0911645 Kadi Namba : 6464093 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/37337/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda Wilaya ya Morogoro**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na...06..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SAID OMARI WA MOROGORO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: FAMILIA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21/01/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 14/01/2022**

---

**AMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakam ya mwanzo ya wilaya Moshi**
**Kituo cha Marangu mkoa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa mirathi Na………../20…………**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU LAZARO LIM MINJA WA**
**……………………**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA HELLEN LAZARO**

**TANGAZO**
**[kanuni ya 5[2] ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama ya Mwanzo]**

Watu wote wanodai kuwa na uhusiano wowote/maslahiyoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hii endapo wakitak kufanya hivyo mnamo tarehe 04 mwezi 02 mwaka 2022 kabla ya mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zinagatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 06 /01/2022

---




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-11

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Akakumbuka maneno ya Diana kuwa hawezi kuwaacha hao wote wawili ghafla kwa sababu wana uwezo wa kipesa na kimamlaka, wanaweza kutafuta chanzo na wakikipata kuwa ni yeye, basi maisha yake yanaweza kuwa hatarini. Mwanya huo ndiyo sasa anautumia Jan kwenye sakata la mpenzi wake kutekwa.

"Mpwa wangu ametekwa na wewe umesikia, wanasema tupeleke kiasi cha shilingi milioni kumi kwenye daraja la Mfugale pale Tazara, leo usiku saa nane, lakini jamaa wamesema tusiwaambie polisi, vinginevyo watamuua. Usingekuwa mpenzi wake nisingekwambia. Kwa sababu wewe ni polisi, lakini nimelazimika kwa sababu pesa zinatakiwa za kuongezea." Afande Marco alihabarishwa.

"Unasikia kijana, usiwe muoga kiasi hicho, nashukuru kwa taarifa hiyo. Wenda tu nyumbani usiwe na wasiwasi. Ikifika usiku, pelekeni hizo pesa na sisi kama Jeshi la Polisi tutakuja pale na kufanya kazi yetu ya kuwatia nguvuni, halafu watatueleza aliyetekwa nyara yuko wapi."

"Lakini afande mchezo unaotaka kuufanya ni wa hatari kwa Diana." Jan alitahadharisha.

"Yule ni mpenzi wangu mimi, nina uhakika hawatomdhuru na mimi hapa ni mkuu wa kituo, nawasialiana na wenzangu kufanya jambo hilo." Marco alimhakikishia Jan kuwa watekaji watatiwa nguvuni na Diana ataokolewa.

Alitoka hapo akiwa amenyong'onyea, hakuwa na uhakika na usalama wa Diana tena. Yeye ndiye aliyepewa kazi ya kupeleka mkoba wenye pesa chini ya daraja la kisasa la Mfugale maeneo ya Tazara majira ya saa nane usiku.

Kabla ya kwenda kwa Afande Marco, alipitia nyumbani kwake Mwananyamala na kabla ya kwenda kwake, alipitia tena nyumbani kwake.

Hakuna aliyejua kuwa ndiye aliyetakiwa kupeleka pesa hizo. Hata hivyo alihofia usalama wake. Kitendo cha watekaji kwenda kuchukua pesa, huku askari polisi nao wakienda kuzuia uchukuaji huo, na kuwakabili kwa ajili ya kuwakamata, alijua kabisa kutakuwa na patashika nguo kuchanika.

Aliporejea kwa mjomba Ken alikwenda moja kwa moja hadi kwenye chumba alichopewa kulala.




**"Kingine mjomba, wewe huwezi kukosa bastola, kama unayo naomba, ujue ni lazima pale wakati unapeleka uwe na angalau kitu ambacho unaweza kujitetea ikitokea."**

Humo pia ndiyo kulikuwa na mkoba wa pesa. Mkoba ambao uliletwa ukiwa na kiasi cha shilingi milioni kumi na tano tu zilizoletwa na tajiri Chala.

Mjomba Ken yeye alitaka kutoa shilingi milioni tano, ili ziwe ishirini, lakini Jan alikataa na kumwambia asifanye hivyo.

"Mjomba hata ukiweka hizo pesa, bado hazitotimia milioni hamsini wanazohitaji watekaji. Baki nazo, hizi hizi tu zinatosha.

Ni kweli wakikuta ziko pungufu inaweza kuwa ni hatari kwa Diana, lakini nakuhakikishia hawatomuua, kwa sababu bado watakuwa na nafasi ya kutuambia tutafute tena pesa. Wakimuua ina maana hawawezi kupata pesa zingine."

Ken alishangazwa na ujanja na akili ya Jan. Kingine kilichomshangaza ni kutoonekana na hofu ya kupeleka hizo pesa, kwa sababu lilikuwa ni jambo la hatari sana.

"Unaweza ukaweka tu mkoba, ukapigwa risasi. Huwezi kujua nani anakuona kwa wakati huo." Aliwaza Ken.

"Kingine mjomba, wewe huwezi kukosa bastola, kama unayo naomba, ujue ni lazima pale wakati unapeleka uwe na angalau kitu ambacho unaweza kujitetea ikitokea."

"Ni kweli, hata mimi niliwaza hivyo. Ninayo, una uwezo wa kuitumia?"

"Mimi tena mjomba, uliza kingine."

"Basi pumzika, ikifika saa tano tumke kwa ajili ya maandalizi."

"Sawa mjomba." Alijibu Jan, huku akijilaza kitandani.

****************************

Kulikuwa na kila dalili ya kunyesha mvua. Mawingu yalikuwa yametanda kwenye baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam. Upepo uliokuwa unavuma, ulionekana kulifukuza joto ambalo ndilo mwenyeji wa jiji hilo. Kibaridi kilijitokeza ambacho kinaweza kusababisha kuwafanya wakazi kutafuta majaketi na makoti.

Hata hivyo kibaridi hicho kwa miji kama Moshi, Arusha, Mbeya, Iringa na Sumbawanga, ingetafsiriwa kuwa ni joto. Wakati huo Ken alikuwa ndani ya gari lake, pembeni akiwa na abiria mmoja, Jan.

Safari ilikuwa ni kwenda kuuweka ule mzigo ambao waliambiwa wauwasilishe chini ya daraja.

Hakukuwa na magari mengi kwenye barabara ya Mandela ambayo inatoka Ubungo, ikipitia Buguruni, ikikutana na Barabara ya Nyerere, maeneo ya Tazara na kuendelea mbele hadi maeneo ya Bandarini.

Alipofika kwenye makutano ya barabara ya Uhuru na Mandela aliweka gari lake kando.

Wote wawili hawakutaka kwenda moja kwa moja hadi kwenye eneo la tukio kwa sababu ingekuwa ni hatari zaidi kwao.

Ni kama kujipeleka mwenyewe kwenye mdomo wa mamba au simba.

"Nakuombea urudi salama kijana." Mjomba Ken alimshika kichwa Jan, mithili ya baba anayemtambikia mwanaye anayekwenda ughaibuni na hata uhakika wa kumuona leo au kesho.

"Usijali mjomba, lililokupata ni letu wote, lazima tupambane, likitokea lolote, basi nitakuwa nimejitoa sadaka kwa ajili ya Diana." Alijibu.

Mjomba hakujibu kitu. Alimwangalia Jan akiwa anatembea hatua kwa hatua kuelekea alikotakiwa aende, akiwa na mkoba wake mkononi.

Ilikuwa ni saa nane kasoro dakika tano usiku, Jan alipowasili chini ya daraja la Mfugale, Tazara, Dar es Salaam.

Sehemu kubwa kulikuwa na taa zilizokuwa zinawaka, lakini eneo ambalo alitakiwa kuziweka kulikuwa na kiza totoro. Ulikuwa ni upande wa kulia, linapoteremkia daraja, kama unakwenda Uwanja wa Ndege.

Kila alipokaribia kufika ndipo alipokuwa akitembea kwa uangalifu zaidi. Masikio yake yalikuwa wazi kusikia chochote kile kisicho cha kawaida, au kufuata.

Bastola yake ilikuwa imefutikwa mbele ya suruali, tayari kwa kuichomoa pale atakapohisi kuna hatari.

Hakutaka kuishika mkononi kwani alihisi ni kama kutangaza shari kwa mtu yoyote atakayemuona.

Jan hakutaka kujidanganya kuwa watekaji watamsubiri aweke mkoba wa pesa, halafu aondoke ili nao waje.

Alijua kabisa kuwa watakuwa wapo hapo muda mrefu na wanamuangalia hatua zote anazozipiga kuelekea kuweka mkoba huo wa pesa, hivyo kukamata bastola kungewafanya wahisi huenda kuna ujanja fulani unataka kufanyika. Na huenda wangemmaliza kabisa.

Aliuweka mkoba taratibu sehemu ambayo alitakiwa auweke. Alisimama kiasi cha nusu dakika kuangalia kama kuna chochote, au kutakuwa na amri yoyote ile, kutoka kwa watu wanaozitaka pesa zile.

Baada ya kuona bado kuna ukimya, alianza kuvuta hatua kadhaa nyuma, baadaye akageuka na kuondoka taratibu sehemu ile ya hatari ambayo aliona ni sawa na kuwa ndani ya tumbo la nyangumi.

Kila alivyozidi kusonga mbele, ndivyo alivyozidi kuongeza mwendo. Kila hatua aliyopiga alijiona anaingia sehemu salama zaidi kuliko mwanzo.

"Wewee, unakwenda wapi?" Alisikia sauti nyuma yake. Mwili ukafa ganzi. Alijua sasa amekwisha. Akili ya kutaka kuchomoa bastola ikamjia. Alisita kwa sababu hakujua sauti hiyo inatoka wapi na ni nani.

"Simama wewe." Ilikuwa amri. Alijishauri, aitii au asitii.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# PRISONS YAIPANIA RHINO RANGERS FA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo amesema ana kazi kubwa ya kikosi chake kupambana kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wa hatua ya 32 bora ya kombe la FA dhidi ya Rhino Rangers.

Prisons watashuka dimbani kesho Jumapili kuwakabili Rhino mchezo utakaopigwa katika uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema baada ya kupoteza mechi yao dhidi ya Azam FC wamefanyia kazi mapungufu na sasa wamejipanga imara kwenda kutafuta ushindi dhidi ya Rhino.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wanahitaji kupata matokeo mazuri na kusonga mbele katika hatua ya 16 bora.

"Ni mechi muhimu ni michezo ya mtoano, tofauti na michezo ya ligi, tunahitaji kwenda kupambana kutafuta ushindi na kurejesha molari kwa wachezaji wangu kutokana na matokeo yaliyopita," alisema Odhiambo.

Alisema wanasahau matokeo waliyopata katika mechi zao za nyuma na kuhakikisha wanapambana kutafuta ushindi katika mchezo huo na kusonga mbele zaidi.

"Rhino Rangers sio timu ya kuibeza, tuna waheshimu wapinzani wetu tutacheza kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunaibuka na ushindi katika mchezo huo," alisema Odhiambo.



Mkurugenzi wa Bendi ya Waluguru Original, Killer Boy kulia akiimba na Amina Remmy katika moja ya maonyesho ya bendi hiyo mjini Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Ngailo matumaini kibao soka la kulipwa Uturuki

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu 'Tembo Warriors', Frank Ngailo ameanza vizuri katika majaribio yake ya kucheza soka la kulipwa nchini Uturuki.

Ngailo ambaye yupo nchini humo kwa ajili ya majaribio ya wiki moja katika klabu ya Azmir BBK, akifuzu vizuri anapata mkataba wa kucheza soka la kulipwa nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka Uturuki, Ngailo alisema siku ya kwanza kwenye mazoezi ilikuwa ngumu kwa upande wake kutokana na hali ya hewa ya nchi hiyo.

Alisema ingawa kulikuwa na baridi kali, lakini aliweza kucheza kwa kiwango kikubwa na kupongezwa na viongozi wa klabu ya Azmir BBK.

"Ilinipa ugumu kutokana na hali ya hewa ya huko kuwa baridi, pia mazoezi wanafanya usiku jambo ambalo sijazoea wakati nipo nyumbani Tanzania," alisema Ngailo.

Alisema ana mshukuru Mungu hadi sasa ana asilimia 70 za kufanikisha kucheza soka la kulipwa kwa sababu tangu ameanza kucheza mechi mbili amefunga mabao mawili na kutoa pasi mwisho nne.

"Nina imani kwa mwenendo huu nitafanikiwa malengo yangu kwa sababu naendelea kupambana kuhakikisha napigania nafasi hii ya kucheza soka la kulipwa," alisema Ngailo.

## Waluguru Original waitwa 'Rock City'

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Waluguru Original yenye maskani yake mjini Morogoro, imepata mwaliko wa kutoa burudani jijini Mwanza, ambapo inatarajia kutumia nafasi hiyo kutanua wigo wa kupata mashabiki wengi zaidi.

Mkurugenzi wa bendi ya Waluguru Original, Killer Boy aliliambia gazeti hili kuwa, onyesho hilo litafanyika wiki ya kwanza ya mwezi ujao ikiwa ni mara kwanza kwa bendi hiyo kufanya vitu vyake Mwanza.

"Hii ni nafasi nzuri kwetu kuonyesha makali yetu, ili kujipatia mashabiki zaidi wa muziki wa dansi kutoka mikoa mbalimbali nchini kutokana na ukweli kwamba tumewahi kwenda mikoa michache tu," amesema Killer.

Amesema, mashabiki wa dansi wamekuwa wakiamini kuwa muziki mzuri ni ule unaopigwa na bendi za Dar es Salaam, kwamba wanataka wawaondoe mawazo hayo kwa kuwa hata nje ya Dar es Salaam kuna bendi nzuri.

## Komba, Ndimbo wa TFF waula CAF

**Na Adam Fungamwango**

MWAMUZI wa kimataifa wa Tanzania, Frank Komba na waamuzi wanne wa kike, pamoja na Ofisa Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Cliford Ndimbo wameteuliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwenda kuchezesha na kuzimamia mechi mbalimbali zinazosimamiwa na Shirikisho hilo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), imesema kuwa CAF imemteua Ndimbo kuwa Ofisa Habari wa mechi kwa hatua ya Makundi Kombe la Shirikisho Afrika kati ya wenyeji Simba watakapoikaribisha Asec Mimosas ya Ivory Coast kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Februari 13 mwaka huu.

Mwamuzi bora kabisa kwa sasa nchini, Kombe, ni miongoni mwa waamuzi watakaochezesha mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kati ya Raja Casablanca ya Morocco dhidi ya Amazulu ya Afrika Kusini, utakaochezwa kwenye Uwanja wa Mohamed wa tano unaotarajia kupigwa Februari 12 mwaka huu.

Taarifa hiyo pia inasema shirikisho hilo la Afrika limewateua waamuzi watatu wa kike wa Tanzania, Tatu Malogo, Janeth Balama na Hellen Mduma kuchezesha mchezo wa Kufuzu Kombe la Dunia kwa Wasichana chini ya miaka 17, kati ya timu ya taifa ya Djibouti dhidi ya Burundi, uliopangwa kuchezwa kati ya Machi 4, 5 au 6 mwaka huu.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VLAHOVIC ATUA JUVE
JUVENTUS wamekubali kumsajili mshambuliaji wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, ambaye amekuwa akihusishwa na Arsenal, kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 62.4. ***(Mail, via Guardian)***

### GUIMARAES RASMI NEWCASTLE
NEWCASTLE United wamekamilisha dili la kumsaini kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 24 kutoka Lyon kwa pauni milioni 30.***(Talksport)***

### MOURINHO UHAKIKA KWA XHAKA
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho ana matumaini kuwa timu hiyo ya Serie A inaweza kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 29, kabla ya dirisha la usajili la Januari kufungwa. ***(Mail)***

***

### WEST HAM YATAKA WAWILI
WALENGWA wawili wakuu wa West Ham katika dirisha la usajili la Januari ni mshambuliaji wa Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko kwa mkopo Southampton kutoka Chelsea, na mshambuliaji wa Chile, Ben Brereton Diaz mwenye miaka 22, anayechezea Blackburn Rovers. ***(Football Insider)***

### BROJA AGOMBEWA
KLABU za Everton, Leeds United na Wolves pia zina nia ya kumsajili Armando Broja, ambaye Southampton wanataka kumbakisha. ***(Teamtalk)***

### LUIZ AWANIWA EPL
ASTON Villa wamekataa dau la pauni milioni 30 kutoka kwa klabu moja ya Ligi ya England ambayo haijatajwa jina kwa ajili ya kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz. ***(Evening Standard)***

### GAKPO KUSUBIRISHWA
MBIO za Arsenal kumsajili Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 22, zitalazimika kusubiri hadi angalau dirisha la majira ya joto, kwani klabu yake ya PSV Eindhoven bado inataka kumbakiza. ***(Mail)***

### TURNER ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal imekubali mkataba wa kumsajili mlinda mlango wa Marekani, Matt Turner mwenye umri wa miaka 27 kutoka klabu ya New England Revolution msimu wa joto.***(Athletic)***

### TIMU ZAMGOMBEA LINGARD
KLABU za Aston Villa, Everton na Leicester City zinamfuatilia mchezaji wa kimataifa wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29. ***(Manchester Evening News)***

### BARCA YAMTAKA MEUNIER
BARCELONA wamefanya mawasiliano na Borussia Dortmund huku wakitafuta kumsajili beki wa kulia wa Ubelgiji, Thomas Meunier mwenye umri wa miaka 30 kwa mkopo. ***(Marca)***

### YOUNG AIKATAA NEWCASTLE
ASHLEY Young wa Aston Villa, ambaye anaweza kucheza kama beki au winga, amekataa kuhamia Newcastle United, huku mchezaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 36 akitaka kubaki Villa Park. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KOCHA BRAZIL ALIA NA MWAMUZI

**Walazimishwa sare na Ecuador, kadi nne nyekundu zatolewa VAR ikikataa mbili na...**

**SAO PAULO, Brazil**

KOCHA Mkuu wa Brazil, Tite ameshutumu maamuzi ya kuteuliwa kwa mwamuzi wa Colombia kwenye mchezo wa Alhamisi uliojaa vurugu nyingi wa sare ya 1-1 dhidi ya Ecuador wa kufuzu kombe la Dunia.

Mwamuzi wa Colombia, Wilmar Roldan alitoa kadi nyekundu nne kwenye mchezo huo, ikiwemo mara mbili kwa golikipa wa Brazil, Alisson ambapo baadae zilikataliwa na VAR, pamoja na penalti mbili kwa Ecuador pia zilikataliwa.

Wakiongoza kwa bao 1-0 lililofungwa na Casemiro kipindi cha kwanza, Ecuador walipata penalti dakika ya 55, lakini baadae ikasitishwa baada ya VAR kuonesha Pervis Estupinan hakufanyiwa faulo la Raphinha kwenye eneo la hatari.

Dakika ya 75 Ecuador walisawazisha kwa bao la Felix Torres kabla ya mwamuzi kutoa tena penalti kwa faulo ya Alisson, lakini VAR ikakataa.

Baada ya mchezo huo, Tite alimshutumu mwamuzi Roldan kwa maamuzi mabaya, lakini pia alihoji uamuzi wa kumtea refa huyo kutoka nchini Colombia ambayo inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa kufuzu kombe la Dunia.

"Leo (juzi) lilikuwa suala la uchaguzi wa mwamuzi kutoka nchi inayoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa kufuzu kombe la Dunia, wakati wanaoshika nafasi ya tatu na ya kwanza wakiwa wanacheza," alisema Tite akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Roldan ni mwamuzi mzuri, lakini uteuzi wake haukuwa sahihi kwa mchezo kama huu."

Tite aliongeza: "Ulikuwa mchezo mgumu. Idadi ya faulo zilikuwa nyingi. Faulo 20 zilifanywa na Ecuador na sisi tulifanya 12.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 878

MECHI KALI
GAMBIA
VERSUS
CAMEROON
1 | 7.14
X | 3.47
2 | 1.56

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TRAORE HUYO BARCELONA



**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imefungua mazungumzo na Wolves kwa ajiili ya kumsajili tena winga wa Hispania, Adama Traore.

Klabu hiyo ya Katalunya inataka kwanza imsajili kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja mwishoni mwa msimu huu.

Hiyo ina maana kwamba, uhamisho wa kwenda Tottenham umekufa kwa mchezaji huyo mweye umri wa miaka 26, ambaye alianza maisha yake ya soka pale Barcelona.

BBC Sport inaelewa kwamba, kikosi cha kocha, Antonio Conte awali kilikuwa kimetoa ofa ya pauni milioni 15 kwa Traore ambayo ilikataliwa wiki iliyopita, ingawa vyanzo kutoka klabu hiyo ya London vilikanusha kutoa ofa hiyo.

Traore amebakiza miezi 18 kwenye mkataba wake wa sasa hapo kwenye dimba la Molineux na mazungumzo kuhusu mkataba mpya hayakufikiwa.

Aliondoka pale Nou Camp kwenda Aston Villa mwaka 2015 na alitumia miaka miwili akiwa Middlesbrough kabla ya kujiunga na Wolves kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 18 mwaka 2018.

Winga huyo amecheza mechi 154 kwa klabu hiyo akifunga mabao 11.

# Kroos ataka kumalizika soka Real Madrid

**MADRID, Hispania**

TONI Kroos amesisitiza anataka kutumia muda wake uliobaki wa kucheza soka katika Klabu ya Real Madrid, huku mkataba wake wa sasa ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Kroos alihamia pale Santiago Bernabeu mwaka 2014 kutoka Bayern Munich na amecheza mechi 344 kwa Los Blancos hao katika mashindano yote, akifunga mabao 25 na kutoa pasi za mwisho 77.

Mjerumani huyo ameshinda mataji mawili ya LaLiga, matatu ya Ligi ya mabingwa Ulaya, mawili ya UEFA Super na manne ya Klabu bingwa ya Dunia tangu alipotua nchini Hispania, na amethibitisha kwamba anapenda kumalizia kipindi chake cha uchezaji hapo Madrid.

"Nataka kumalizika kipindi changu cha uchezaji hapa," alisema Kroos katika mahojiano na RTVE.

"Familia yangu na mimi mwenyewe tunajisikia furaha kuwa Madrid, bado kuna mwaka mmoja umebaki kwenye mkataba wa sasa."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 pia amzungumzia kuhusu msimu huu katika mbio za kuwania ubingwa wa LaLiga, huku Madrid wakiwa wanaongoza msimamo kwa pointi nne dhidi ya Sevilla waliopo nafasi ya pili akisema: "Tunatakiwa kuchukua pointi zote kwenye Ligi, bado kuna nyingi zimebaki."



HABARI MICHEZO


,152,880

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/01/22 | 18:00 | Amorebieta vs Girona | 2.80 | 3.09 | 2.50 |
| 02. 29/01/22 | 18:00 | Tranmere vs Forest Green | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 03. 29/01/22 | 18:00 | Oldham vs Rochdale | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 04. 29/01/22 | 18:15 | Nancy vs Amiens | 2.52 | 3.16 | 2.77 |
| 05. 29/01/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Almeria | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 06. 29/01/22 | 18:30 | SBV Excelsior vs Emmen | 2.56 | 3.49 | 2.46 |
| 07. 30/01/22 | 16:30 | Vicenza vs Alessandria | 2.66 | 3.05 | 2.66 |
| 08. 30/01/22 | 18:30 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 09. 30/01/22 | 18:30 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.90 | 3.20 | 2.47 |
| 10. 30/01/22 | 19:00 | Cardiff vs Nottingham | 2.55 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 30/01/22 | 20:30 | PAOK vs Olympiakos | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 12. 30/01/22 | 23:00 | Lens vs Monaco | 2.77 | 3.26 | 2.46 |
| 13. 30/01/22 | 23:00 | Ponferradina vs Tenerife | 2.42 | 3.11 | 2.91 |

## MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 29/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 3460 | Ross County vs Rangers | 7.70 | 4.74 | 1.36 |
| 15:45 | 3185 | KuPS Kuopio vs VPS Vaasa | 1.25 | 5.02 | 9.65 |
| 16:00 | 1233 | Hapoel Katamon vs Hapoel Beer Sheva | 5.97 | 3.80 | 1.49 |
| 16:00 | 1867 | Konkola Blades vs Zanaco | 3.23 | 2.66 | 2.41 |
| 16:45 | 4236 | Persib Bandung vs PS Tni | 1.77 | 3.41 | 4.13 |
| 17:30 | 4055 | Flint Town United vs Cardiff Met Uni. | 1.71 | 3.80 | 3.95 |
| 17:30 | 5304 | Gap Connahs Quay vs Barry Town FC | 1.49 | 4.35 | 5.03 |
| 18:00 | 1222 | Crusaders Belfast vs Glenavon | 1.26 | 5.39 | 8.27 |
| 18:00 | 1400 | Lahti vs Haka | 2.70 | 3.18 | 2.41 |
| 18:00 | 1470 | Hibernian vs Livingston | 1.78 | 3.40 | 4.53 |
| 18:00 | 1884 | Barnsley vs Bournemouth | 4.79 | 3.66 | 1.67 |
| 18:00 | 2090 | Millwall vs West Bromwich | 3.29 | 3.14 | 2.19 |
| 18:00 | 2206 | Aberdeen vs St Johnstone | 1.67 | 3.54 | 5.12 |
| 18:00 | 2325 | Clinceni vs Farul Constanta | 44.40 | 9.87 | 1.05 |
| 18:00 | 2531 | Middlesbrough vs Coventry | 2.08 | 3.25 | 3.44 |
| 18:00 | 2596 | Queen of South vs Dunfermline | 2.53 | 3.11 | 2.72 |
| 18:00 | 2792 | Glentoran Belfast vs Warrenpoint | 1.13 | 7.14 | 13.51 |
| 18:00 | 2911 | Coleraine FC vs Linfield Belfast | 3.37 | 3.18 | 2.04 |
| 18:00 | 2934 | Dundee FC vs St Mirren | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 18:00 | 3060 | Arbroath vs Partick Thisle | 2.43 | 3.12 | 2.83 |
| 18:00 | 3127 | Fulham vs Blackpool | 1.28 | 5.29 | 9.01 |
| 18:00 | 3561 | Preston vs Bristol City | 1.86 | 3.34 | 4.13 |
| 18:00 | 3843 | Hull City vs Swansea | 2.65 | 3.09 | 2.65 |
| 18:00 | 3855 | Kilmarnock vs Inverness | 2.09 | 3.22 | 3.37 |
| 18:00 | 4116 | Celtic vs Dundee Utd | 1.12 | 7.68 | 18.70 |
| 18:00 | 5008 | Amorebieta vs Girona | 2.98 | 3.08 | 2.38 |
| 18:00 | 5062 | Luton Town vs Blackburn | 2.35 | 3.13 | 2.99 |
| 18:00 | 5498 | Hamilton vs Ayr United | 2.04 | 3.31 | 3.41 |
| 18:00 | 5719 | QPR vs Reading | 1.49 | 4.21 | 5.87 |
| 18:00 | 5824 | Hearts vs Motherwell | 1.68 | 3.65 | 4.83 |
| 18:15 | 2138 | Nancy vs Amiens | 2.52 | 3.11 | 2.81 |
| 18:15 | 3593 | Toulouse vs FC Versailles 78 | 1.22 | 5.90 | 11.79 |
| 18:15 | 4362 | Kfco Wilrijk vs Zulte Waregem | 2.30 | 3.51 | 2.82 |
| 18:30 | 1447 | FC Ashdod vs Maccabi Tel Aviv | 4.83 | 3.72 | 1.60 |
| 18:30 | 3733 | SBV Excelsior vs Emmen | 2.56 | 3.49 | 2.46 |
| 19:00 | 4465 | Nazareth Ilit vs Maccabi Petach Tikva | 2.93 | 3.17 | 2.26 |
| 19:05 | 1583 | HNK Sibenik vs Hajduk Split | 5.58 | 4.14 | 1.47 |
| 20:00 | 5197 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.03 | 3.64 | 3.24 |
| 20:30 | 2241 | RFC Seraing vs Eupen | 2.41 | 3.35 | 2.76 |
| 20:30 | 2973 | Larne vs Portadown FC | 1.16 | 6.58 | 11.60 |
| 20:30 | 3018 | Reims vs Bastia | 1.83 | 3.40 | 4.24 |
| 20:30 | 4885 | Peterborough vs Sheffield Utd | 3.73 | 3.43 | 1.92 |
| 20:50 | 4430 | Hapoel Haifa vs Beitar Jerusalem | 1.84 | 3.42 | 3.80 |
| 21:30 | 2735 | Budapest Honved vs Gyirmot FC | 1.58 | 3.82 | 4.83 |
| 22:00 | 2393 | Burkina Faso vs Tunisia | 3.37 | 2.82 | 2.39 |
| 22:30 | 1959 | BSC Young Boys vs FC Lugano | 1.42 | 4.63 | 6.50 |
| 22:45 | 5333 | Cercle Brugge vs Oostende | 1.52 | 4.24 | 5.52 |
| 23:00 | 2912 | Marseille vs Montpellier | 1.52 | 4.04 | 5.92 |
| 23:00 | 2929 | FC Aguablanca vs Valledupar FC | 1.97 | 3.24 | 3.53 |
| 23:00 | 4011 | Real Oviedo vs Almeria | 2.66 | 3.05 | 2.66 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# JULIANA ATINGA SHINDANO LA FUTURE FACES AFRICA 2022

**Na Dennis Fussi**

MREMBO Juliana Rugumisha amepata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Future Faces Africa Grand Finale 2022 yanayofanyika kesho Lagos, Nigeria.

Juliana ambaye ni Miss Tanzania 2021 amepata nafasi hiyo ambapo washindi 12 watakaopatikana wataingia mkataba wa miaka miwili na kampuni ya FFA katika masuala ya mitindo.

Future Face imejikita katika kutafuta wanamitindo ndani ya Afrika na kushiriki katika shindano hilo la kipekee na mfano ni moja ya mashindano makubwa kuwahi kutokea barani humu.

Mwanzilishi wa FFA na mmiliki wa moja ya wakala mkubwa wa mitindo Afrika, Elizabeth Elohor, amesema katika miaka iliyopita Dunia imeshuhudia ongezeko kubwa la kutambuliwa na kuthaminiwa kwa wanamitindo wa kiafrika na mitindo yake ikipatiwa nafasi kubwa.

Alisema washindani 12 wanaoshindania nafasi ya kushinda mkataba wa mitindo ya kimataifa ya miaka miwili na wakala wa juu wa uanamitindo wa kimataifa na washindi watazawadiwa fedha taslimu dola 5,000 za Marekani ambazo ni sawa na Sh Milioni 11 za Tanzania kwa washindi wa kiume na wa kike.

Aliongeza walitamani kufika Tanzania, lakini mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona umekuwa ni changamoto, lakini anaamini mwaka 2024 watafika kutafuta vipaji vipya hapa nchini.

Naye Millen Magese aliyekuwa Miss Tanzania 2001 ambaye ni mwanamitindo wa kimataifa anayeishi jijini New York nchini Marekani na pia Mkurugenzi wa MMG, alisema hii ni fursa nyingine kwa wanamitindo kwa bara la Afrika.

"Hii ni nafasi nyingine na kubwa zaidi kwa vijana wetu wa kike na kiume, mwaka huu umeenda mshiriki mmoja, mwakani vijana wajipange kwa ajili ya kushiriki na wadhamini wajitokeze kwa ajili ya kuunga mkono mashindano hayo," alisema Magese.

Kwa upande wa mrembo Juliana alisema amejiandaa vizuri kuipeperusha bendera ya Tanzania na anaamini ataweza kuibuka kuwa mmoja wa washindi.

# Ligi daraja la kwanza kuunguruma leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI daraja la Kwanza kanda ya Unguja inaendelea leo, baada ya kusimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi pamoja na dirisha dogo la usajili.

Leo itapigwa michezo miwili katika viwanja tofauti kwa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja, ambapo kwenye uwanja wa Kitogani Wenyeji Paje Star watacheza dhidi ya Chuoni.

Mchezo wa pili utapigwa katika uwanja wa Kinyasini Mkoa wa Kaskazini utawakutanisha Wembe FC dhidi ya Gulioni FC.

Michuano ya ligi daraja la kwanza kanda ya Unguja timu nne zitashuka daraja kuelekea ligi za mikoa yao na timu nne zitapanda daraja na kucheza Ligi Kuu ya Zanzibar msimu ujao wa 2022-2023.

Kwa mujibu wa kanuni ya mashindano msimu huu, kila kanda itapandisha timu mbili ambazo ni Pemba na Unguja ili kupata jumla ya timu nne za Ligi Kuu.

Michezo
Jumamosi Januari 29, 2022
Nipashe

UKURASA 21

Kocha Brazil alia na mwamuzi





Wachezaji wa Yanga wakifanya mazoezi kwenye uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana, kujiandaa kwa ajili ya mchezo wa kombe la FA dhidi ya Mbao FC utakaopigwa leo kwenye dimba hilo. **PICHA:YANGA**

# YANGA YAIKABILI MBAO

●●●Ni mchezo wa kombe la FA hatua ya 32 bora leo, Bumbuli asema wataingia uwanjani kwa tahadhari bila dharau na kikosi kiko fiti kuondoka na...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo watashuka kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza kucheza mechi ya hatua ya 32 bora ya Kombe la FA dhidi ya Mbao FC.

Awali mechi hiyo ilikuwa ichezwe kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, lakini kwa sababu una matumizi mengine, ulipelekwa kwenye uwanja huo ambao ni nyumbani kwa Mbao, ingawa Yanga ndiye mwenyeji.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli amesema kuwa maandalizi ya mechi yamekamilika na kinachosubiriwa ni dakika 90, na wao wamejipanga kushinda mechi hiyo.

"Maandalizi ya mechi hii yalianza mapema, ndiyo maana tulicheza na Mbuni FC ambayo ipo Ligi Daraja la Kwanza kama ilivyo kwa Mbao na kocha wetu, Nasreddine Nabi ameshajipanga vizuri kwa mchezo huu," alisema Bumbuli.

Mechi hiyo ya kirafiki ilichezwa Januari 19 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha na Yanga kushinda mabao 2-0 yote yakifungwa kwa penalti zilizopigwa na Mukoko Tonombe ambaye ilikuwa mechi ya mwisho kwake, kabla ya kutimkia TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Bumbuli alisema kuwa Yanga ambayo imefika jijini Mwanza na wachezaji 19, haina majeruhi yoyote na wanaingia kamili bila kudharau mechi hiyo.

"Tunaingia bila kuidharau Mbao kwa sababu, kwanza imefika hapo kwa kupata matokeo mazuri, lakini mchezo huu ni wa mtoano, hivyo ukipoteza unatolewa," alisema.

Hata hivyo, Yanga itacheza mechi hiyo bila kocha wake msaidizi, Cedric Kaze benchini ambaye amerejea nchini Burundi baada ya taarifa za mkewe kujifungua.

"Kaze ana ruhusa ya wiki moja, amekwenda kumuona mtoto wake, mkewe amejifungua, amerejea Burundi, lakini atauwahi mchezo wa raundi ya 14 ya Ligi Kuu dhidi ya Mbeya City.".

Mmiliki wa Mbao FC, Ammy Ninje amesema wamejidhatiti kuikabili Yanga, na wamefurahi mechi kupelekwa CCM Kirumba.

"Mpira wa Tanzania kuanzia Ligi Kuu hadi Daraja la Kwanza uko sawa tu, kinachobadilika ni suala la kifedha, lakini pale uwanjani watu 11 kwa 11, wote wanakuwa sawa tu. Mtaona wenyewe tumejiandaa, tuko vizuri kuikabili Yanga na naamini tutawatoa na kusonga mbele," alisema Ninje.

Yanga ilifika hatua ya fainali msimu uliopita, lakini ikafungwa bao 1-0 na watani zao wa jadi, Simba Julai 25 mwaka jana kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma bao likifungwa na Thadeo Lwanga.

# Pablo atuliza hali ya hewa Simba SC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco ametuliza hali ya hewa ndani ya klabu hiyo na kusema katika nyakati mbaya familia hukaa pamoja, wenye busara hutulia, kujiimarisha na kupanga namna ya kushinda vita vinavyofuata mbele yao.

Simba iko katika maandalizi ya mchezo wa hatua ya 32 bora ya kombe la FA dhidi ya Dar City utakaopigwa kesho katika dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Pablo amesema siku tisa kwao zimekuwa ngumu ambapo wamecheza mechi tatu za ugenini zilizowafanya kusafiri umbali mrefu bila matokeo.

Alisema ratiba ilikuwa ngumu na imesababisha wachezaji kuchoka huku wengine wakipata majeraha ambayo yamewafanya kukosa baadhi ya mechi.

"Mchezo dhidi ya Kagera Sugar timu yetu ilibadilika kiuchezaji kwa kutengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini hatukuzitumia vizuri,"alisema Pablo.

Aliongeza; "Sasa ni wakati wa kutulia, kuungana na kutafakari nini cha kufanya ili kulimaliza tatizo hili."

Alisema kulingana na hali wanayopitia hata familia hukaa pamoja, wenye busara hutulia na kuonyesha ushujaa kujiandaa kushinda vita vinavyowakabili mbele yao.

Wakati kocha akitoa kauli hiyo wazee wa kwa klabu hiyo ya wekundu wa Msimbazi wakiongozwa na mwenyekiti wa zamani wa timu hiyo, Hassan Dalali wanatarajia kukutana na viongozi wa timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dalali alisema lengo kuu la kukutana ni kujadiliana mambo mbalimbali kuhusu mwenendo wa timu yao na hali wanayopitia sasa.

Alisema kikao wanachokifanya ni cha kawaida na watakutana na viongozi wa klabu hiyo kuangalia nini kinachosumbua timu yao kwa mwenendo wanaopita kwa kupoteza pointi nane katika michezo miwili.

"Tunakutana kujadiliana kulingana na mwenendo wa timu yetu, tutatoa ushauri wetu kwa uongozi na wao tuwasikilize maoni yao nina imani tunaweza kupata ufumbuzi katika hilo," alisema Dalali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042